

**MATUMIZI YA TASFIDA ZA KUJAMIIANA NA USAWIRI WA JINSIA  
KATIKA KIPINDI CHA CONNECT CHA RUNINGA YA K24, KENYA**

**ANNE NJAMBI CHEGE**

Ripoti hii imewasilishwa Kwa Graduate School Kwa Madhumuni ya Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili Katika Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Egerton

**CHUO KIKUU CHA EGERTON  
APRILI, 2016.**

## **UNGAMO NA IDHINI**

### **UNGAMO**

Ripoti hii ni kazi yangu binafsi na haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji yoyote ya shahada katika Chuo Kikuu kingine.

Sahihi ..... Tarehe.....

Anne Njambi Chege

AM12/2988/11

### **IDHINI**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii walioteuliwa na Chuo Kikuu Cha Egerton.

Sahihi..... Tarehe.....

Prof. Onyango Ogola

**Idara ya Fasihi, Lugha na Isimu.**

**Chuo Kikuu cha Egerton.**

Sahihi..... Tarehe.....

Dr. Mayaka Gwachi

**Idara ya Fasihi, Lugha na Isimu.**

**Chuo Kikuu cha Egerton.**

## **HATILINZI**

©Anne Njambi Chege 2016

Kazi hii au sehemu yake haikubaliwi kamwe kunukuliwa kwa namna yoyote bila idhini ya mtafiti au Chuo Kikuu cha Egerton. Atakayefanya hivyo atakuwa na hatia na attachakuliwa hatua ya kisheria.

## **TABARUKU**

Kwa mume wangu mpenzi na rafiki

Musa k. Langat

Kwa upendo na uvumilivu wako usio na kifani.

Na kwa watoto wangu wapendwa

Jeremy, Brian na John.

## **SHUKRANI**

Kwanza namtolea mungu shukrani kwa kunilinda, kuniwezesha na kuniongoza katika kazi hii. Shukrani zisizomithilika ziwaendee wasimamizi wangu Prof. Onyango Ogola na Dkt. Mayaka Gwachi. Hakika mlilitolea kuniongoza, kunishauri na kunihimiza. Asanteni kwa uvumilivu wenu. Ningependa pia kuwashukuru wahadhiri wote walionifunza wakiwemo Dkt. Chai, Dkt. Nabea, Prof. Onyango, Dkt. Mayaka na Prof. Kitetu.

Nawashukuru pia wanafunzi wenzangu tulioshirikiana pamoja tangu mwanzo wa masomo yetu. Hawa ni Alomo, Amunga, Micheni, Guyano, Alice, Grace, Caroline, Ruth, Catherine na Jerop. Shukrani za kipekee zimwendee Alice ambaye amekuwa rafiki yangu na tulihimizana.

Namshukuru mume wangu mpPENDWA Bw. Musa Langat kwa kunihimiza na kunitia moyo niendeleze masomo yangu. Nashukuru kanisa la JGC Bomet likiongozwa na kasisi Gilbert Mutai kwa kuniombea na kusimama nami katika kazi hii.

Nawashukuru watoto wangu Jeremy, Brian na John kwa kuvumilia kutoshughulikiwa na mama wakati nilikuwa nikifanya utafiti, asanteni sana.

Namshukuru mamangu Magret Chege kwa kuniombea na kunihimiza nijikaze.

Shukrani zangu pia ziwaendee ndugu yangu Kehio na mkewe Wambui, dada zangu Penina, Njeri, Wambui, Sarah, Wangui na Wanjiru.

## IKISIRI

Swala la kujamiihana katika jamii za Kiafrika huchukuliwa kama swala zito na la aibu na halifai kujadiliwa hadharani. Ni mwiko kutaja misamiati ya sehemu nyeti za mwili na kitendo chenyewe cha kujamiihana. Tasfida ina dhima kubwa kuonyesha jinsi watu wanavyoona mambo na kuunda uhalisia katika fikira zao na husaidia kupunguza makali ya maneno tunayoyatumia. Tasfida hutumiwa kwa wingi na huwa ni za aina mbalimbali. Kipindi cha *Connect* kinatumia tasfida mbalimbali, lakini hatujapata kujua ni tasfida za aina gani zinazotumiwa na zinasawiri nini katika matumizi yazo. Utafiti huu ulidhamiria kushughulikia madhumuni yafuatayo; Kwanza, kutambua na kueleza tasfida za kujamiihana zinazotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha K24. Pili, kujadili swala la jinsia katika tasfida za kujamiihana zinazotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24. Utafiti huu ulidhamiria kujibu maswali yafuatayo: Kwanza, ni tasfida zipi zilizotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24 na zilitolewa maelezo yapi? Pili, swala la jinsia katika tasfida zilizotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24 linadhihirikaje? Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi (UHU) ambayo nguzo zake ni itikadi, uwezo na uhakiki. Utafiti huu ulifanywa maktabani na nyanjani. Maktabani ulihusu udurusu wa vitabu, tasnifu, majarida na huduma za mtandao. Nyanjani ulihusu ukusanyaji wa data kwa kuhusisha utazamaji, mahojiano na kurekodi. Vyombo vyta utafiti vilivyotumiwa ni kinasa sauti na kanda za kunasa sauti. Uchanganuzi wa data ulikuwa wa kimaelezo, kuchanganua tasfida mbalimbali zinazotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24. Mbinu ya utazamaji na kudondoa tasfida za kujamiihana kutoka kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24 zilitumika. Tasfida hizo zilitolewa maana na kuzichanganua jinsi zilivyodhihirisha au zilivyo sawiri jinsia. Utafiti huu ulibainisha wazi kuwa kuna tasfida za kujamiihana zilizotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24 na kuwa tasfida hizo zilidhihirisha au zilisawiri jinsia, hivi kwamba mwanamume amesawiriwa kichanya ilhali mwanamke kihasi. Utafiti huu utasaidia wakufunzi wa maswala ya jamii kujua umuhimu wa kutumia tasfida badala ya lugha ya moja kwa moja, wanapotoa mafunzo ya aila. Utasaidia katika uwanja wa isimu hasa pragmatiki na semantiki kwa sababu unajihuisha na jinsi lugha inavyotumiwa katika jamii. Pia utawanufaisha wasomi kuhusu masuala ya kijinsia na vilevile watafiti wanaotumia nadharia ya uchanganuzi hakiki usemi.

## ABSTRACT

Sexuality in the African society is a serious and an embarrassing issue and it is not supposed to be discussed in the open. It is a taboo to utter tabooed words or the act of sex. Euphemisms play a great role in the way people view issues and the way they construct reality in their mind. They help to reduce the impact of the tabooed words that we use. Euphemisms are mostly used and are of different types. *Connect* is a program that uses different types of euphemisms, but we do not know the types used and what they portray in their use. This research aims at dealing with the following objectives; One, to identify and discuss sexual euphemisms used in the program of *Connect* of K24 television. Two, discuss gender issues in those sexual euphemisms used in program of *Connect* of K24 television. It addresses the following questions: Which euphemisms were used in the program *Connect* and their interpretations? Discuss gender issues in euphemisms used in the program *Connect* of K24 television? This research used Critical Discourse Analysis (CDA) theory which main pillars are ideology, power and criticality. This research was done in the library and field. In the library there was perusing of books, thesis, magazines and internet. In the field there was collecting of data through observation, interview and recording sound recorders and CDs were used. The qualitative method of data analysis was used. There was analysis of euphemisms that were used in the program of *Connect* of K24 television. The method of watching and collecting euphemisms of sex from the program of *Connect* of K24 television was used. Analysing of meaning of those euphemisms and how they portray gender was done. This research showed that there are sexual euphemisms used in the program *Connect* of K24 television and they portray gender, in that man is portrayed positively while woman negatively. It will help teachers and commentators of social issues to know the importance of using euphemisms instead of using direct languages in their teachings on families. This research is important since it would help in the linguistic field especially in pragmatics and semantics because it concerns the use of language in the society. It will also help scholars in gender issues and researchers who use Critical Discourse Analysis theory (CDA).

## YALIYOMO

<b>UNGAMO NA IDHINI .....</b>	<b>ii</b>
<b>UNGAMO .....</b>	<b>ii</b>
<b>IDHINI .....</b>	<b>ii</b>
<b>HATILINZI .....</b>	<b>iii</b>
<b>TABARUKU .....</b>	<b>iv</b>
<b>SHUKRANI .....</b>	<b>v</b>
<b>IKISIRI .....</b>	<b>vi</b>
<b>ABSTRACT .....</b>	<b>vii</b>
<b>YALIYOMO.....</b>	<b>viii</b>
<b>SURA YA KWANZA.....</b>	<b>1</b>
<b>UTANGULIZI.....</b>	<b>1</b>
1.0 Usuli wa Mada .....	1
1.1 Suala la utafiti .....	4
1.2 Madhumuni ya Utafiti .....	4
1.3 Maswali ya Utafiti.....	4
1.4 Umuhimu wa Utafiti .....	5
1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti .....	5
1.6 Maelezo ya Istilahi .....	6
<b>SURA YA PILI.....</b>	<b>7</b>
<b>MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA .....</b>	<b>7</b>
2.2 Mapitio ya maandishi.....	7
2.2.1 Dhana na Dhima ya Tasfida .....	7
2.2.2 Lughah, Kujamiihana na Jinsia .....	10
2.2.3 Mawasiliano ya Runinga.....	17
2.3 Misingi ya Nadharia .....	20
<b>SURA YA TATU .....</b>	<b>25</b>
<b>MBINU ZA UTAFITI.....</b>	<b>25</b>
3.1. Utangulizi.....	25
3.2 Mahali pa Utafiti .....	25
3.3 Kundi la Utafiti au Walengwa.....	25
3.4 Uteuzi wa Sampuli .....	25
3.5 Muundo wa Utafiti .....	26

3.6 Ukusanyaji wa Data .....	26
3.7 Uchanganuzi wa Data .....	27
<b>SURA YA NNE.....</b>	<b>28</b>
<b>UCHANGANUZI WA DATA NA MATOKEO YA UTAFITI .....</b>	<b>28</b>
4.1 Utangulizi.....	28
4.2 Tasfida.....	28
4.2.1 Tasfida za Kuumeni .....	28
4.2.2 Tasfida za Uukeni .....	29
4.2.3 Tasfida za Mitindo au Jinsi ya Kujamiiana .....	30
4.2.4 Tasfida za Tendo la Kujamiiana .....	32
4.2.5 Tasfida Nyinginezo .....	33
4.3 Mwasilishaji na Muktadha wa Matumizi ya Tasfida .....	34
4.4 Usawiri wa Jinsia katika tafsida .....	46
4.5 Matokeo ya Utafiti .....	55
<b>SURA YA TANO.....</b>	<b>57</b>
<b>MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....</b>	<b>57</b>
5.1 Utangulizi.....	57
5.2 Muhtasari wa Tasnifu.....	57
5.3 Hitimisho.....	58
5.4 Mapendekezo .....	58
<b>MAREJELEO .....</b>	<b>59</b>
<b>VIAMBATISHO .....</b>	<b>66</b>
<b>KIAMBATISHO A. MAHOJIANO .....</b>	<b>66</b>
<b>KIAMBATISHO B.....</b>	<b>67</b>

## **ORODHA YA MAJEDWALI**

Jedwali la1: Sampuli ya vipindi vilivyoteuliwa.

Jedwali la 2: Tasfida za kurejelea kuumeni.

Jedwali la 3: Tasfida za kurejelea ukeni.

Jedwali la 4: Tasfida za mitindo ama jinsi ya kujamiihana.

Jedwali la 5: Tasfida za tendo la kujamiihana.

Jedwali la 6: Tasfida nyinginezo.

## SURA YA KWANZA

### UTANGULIZI

#### 1.0 Usuli wa Mada

Kujamiihana ni suala zito mno katika ndoa na huzua mgogoro katika familia nyingi. Asilimia kubwa ya talaka zinazotokea, kiini chake huwa ni kuhusiana na kujamiihana. Watu wengi huhofia na hukwepa kuzungumzia swala hili kwa sababu katika jamii nyingi za Kiafrika huwa ni mwiko. Aswani na wengine (2006) wanatafsili mwiko kama jambo lililokatazwa katika jamii na watu wa jamii hiyo. Malezi ya mke na mume huwa ni tofauti na wengi wao huwa wana utofauti kutokana na mazingira yao tofauti. Pia kuna tofauti ya mtoto wa kike na kiume, kutokana na tofauti za kijinsia. Ni vigumu kukutana na mke na mume ambao wanaafikiana kwa mambo yote.

Kuzungumzia swala la kujamiana kwa lugha ya wazi ni jambo la aibu. Elimu ya familia inatakikana ili kujenga familia yenyeye nguvu na waliooana wafurahie maisha ya ndoa. Hii ni kwa sababu watu wengi, hasa vijana, wanahofia kuingia katika ndoa kutokana na kutopata elimu kuhusiana na ndoa na pia talaka ambazo zinatokea kwa wingi. Wataalamu wengi wamezungumzia elimu ya kujamiihana. Moore na Rosenthal (1993) wanaeleza kuwa mienendo mizuri na uhusiano mzuri katika kujamiihana utafanikiwa ikiwa walimu watazingatia imani ya hadhira lengwa. Wanaendelea kusema kuwa, ufahamu utasaidia vilivyo kuingilia kati na kubadili mienendo na tabia. Undie, Crichton na Zulu (2006) wanasesma kuwa muktadha wa tamaduni za kijamii umetambulika kama muhimu katika kuelewa mienendo ya kujamiihana na lugha; walakini, umepuuzwa ingawa ni muhimu kama kipengele kikuu cha utamaduni. Wanaendelea kusema kuwa lugha huonyesha na kuunda uelewa wa watu kuhusu kujamiihana na maswala mengine. Kwa hivyo, hawa wanasitiza kuwa lugha inapotumiwa katika muktadha wa kitamaduni itasaidia kuelewa maswala ya kujamiihana.

Kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24 ni kipindi cha kipekee ambacho hasa hushughulikia maswala ya familia. Nchini Kenya kuna vipindi mbalimbali vinavyoshughulikia maswala ya uhusiano wa familia katika runinga ya citizen kuna vipindi kama vile mother in law, Papa Shirandula na Machachari. Mother in Law nikipindi kinachoshughulikia uhusiano wa mama mkwe na Bintiye. Mama mkwe ambaye ndiye mamake Charli (Charity) hamtaki mkewe Charli (selina) anamwonyesha madharau

sana ilhali anawapendelea mkewe Robert na watoto wa mwanaye mkubwa. Papa Shirandula nkipindi cha vichekesho kati ya Papa na mkewe Wilbroda wanasumbuana sana. Pia Njoroge rafikiye Shirandula na mkewe wanaosumbuana sana, kwa kutowajibika kwa Njoroge. Machachari ni kipindi cha uhusiano kati ya wazazi na watoto. Katika runinga ya KBC kuna ‘Vitimbi’ kipindi ambacho hujumuisha vichekesho kati ya bwana Ojwang’ na mama Kayai wakiwa bwana na bibi katika familia.

Katika runinga ya K 24 kuna kipindi kama vile ‘The Couples ‘ambacho huhusisha bibi na bwana kutoka familia tofautitofauti. Wao huulizwa maswali na familia ambayo hujibu maswali vizuri hutunukiwa zawadi. Pia kuna kipindi cha sirikal ya bibi ambacho huonyesha upiganiaji wa mamlaka na uwezo katika familia. Bibi huonekana akiwa na uwezo wa kumtawala bwana. Kinyume na mambo yalivyo, kipindi cha *Connect* hujihusisha na maswala ya kujamiihana katika familia, jambo ambalo halijitokezi katika vipindi vingine vya runinga. *Connect* hutumia lugha ya tasfida ilhali vipindi vingine hutumia lugha ya moja kwa moja na ya kawaida.

Kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24 kilibusu mafunzo ya kijamii. Kilishughulikia maswala yanayoongeza mapenzi katika familia na kuwafanya mke na mume kuyafurahia maisha ya unyumba. Familia nyingi zinavunjika na kutalakiana kutohukana na maswala madogo yasiyo na mashiko. Ikiwa maswala haya yanaweza kushughulikiwa wanandoa wataishi vizuri na kufurahia maisha ya ndoa. Kipindi hiki kilijihuhsisha na maswala kama vile njia za kufanya mapenzi, lugha ya mapenzi, mawasiliano katika ndoa, usafi katika ndoa na kadhalika.

Mwasilishi alielezea kuwa njia za kufanya mapenzi ni nyingi. Alielezea kuwa si vizuri wanandoa kutumia njia moja wanapofanya ngono. Anasema ni vizuri kufurahia ngono kwa kutumia njia mbalimbali ambazo zitafanya kujamiihana kufurahiwa na kusichoshe. Alielezea haya kwa kutumia picha za video ambazo wanapozitazama wanawenza kujifunza zaidi.

Akijadili kuhusu lugha ya mapenzi, alieleza kuwa ni vema bibi na bwana waelewe lugha zao za mapenzi. Alisema ni muhali mke kujua kile mumewe anachopenda na mume kujua kinachomfurahisha mkewe. Alisema kuwa ni vema wakati mwingine kuwa na matembezi ya kujamiihana (sex picnic). Huu huwa ni wakati wa kujadiliana maswala ya kifamilia katika mazingira mageni. Matembezi kama haya husaidia kuwaleta wanandoa pamoja zaidi.

Mawasiliano katika familia ni muhimu sana. Mwasilishi alisema ni muhimu wanandoa kuzungumziana. Ni kutokana na mawasiliano ambapo mume au mke atajua anachokipenda na asichokipenda mkewe au mumewe. Mawasiliano pia yatasaidia kujua matarajio au matamanio ya mume na mke. Kuwasiliana kunasaidia kuweka mambo wazi na kukiwa na tatizo litaweza kutatuliwa.

Kuhusiana na usafi katika ndoa. Mwasilishi alielezea kuhusu usafi wa nje na ndani wa mume na mke. Alieleza kuhusu vifaa vya kutumia katika kudumisha usafi. Anaelezea jinsi ya kunyoa na matumizi ya karatasi spesheli ya msalani. Alieleza jinsi ya kujitayarishia kitendo cha kujamiihana na kusema kuwa lazima mwanamke aoge mara mbili kwa siku.

Mwasilishi pia alizungumzia swala la matumizi ya fedha. Alisema matumizi ya fedha ni swala nyeti ambalo limefanya familia nyingi kutengana. Mume na mke lazima waketi chin kujadiliana jinsi ya kutumia pesa wanazozipata. Yafaa wawe na bajeti ya matumizi. Ikiwa ni maendeleo ya kifamilia wajadiliane na wafanye pamoja kama familia. Ni vema kusiwe na miradi ya siri katika familia. Lazima mume na mke wajue miradi yote inayoendelezwa katika familia. Utafiti wetu ulijihusisha tu na tasfida zilizotumika katika swala la kujamiihana katika jamii.

Tafiti nyingi zimefanywa kuhusiana na kujamiihana na athari zake katika kueneza ugonjwa wa ukimwi. Kwa mfano Onyango ametafiti kuhusu uwezo kiume katika vita dhidi ya ugonjwa wa ukimwi nchini Kenya mwaka wa 2011. Njenga, (2011) amefanya utafiti kuhusu matumizi ya istiari kati ya wanafunzi wa chuo kikuu wanaporejelea maswala ya kujamiihana na athari zake katika kueneza ugonjwa wa ukimwi. Berges, Neidebach na Rubin (1983) na Jay, King na Duncan (2006) wameeleza jinsi wazazi wana wasiwasi sana kutumia maneno ya ngono wakiwa na watoto. Katika utafiti wetu tulionyesha tasfida anazotumia mwasilishaji wa kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24 akirejelea maswala ya kujamiihana katika kipindi.

Adei, (1991) ametafiti kuhusu siri ya ndoa yenye furaha (*The Secret of Happy Marriage*), Christensen, na Miller, (2006) wametafiti kuhusu “Areas of desired change among married midlife individuals”. Swala letu la utafiti ni matumizi ya tasfida za kujamiihana na usawiri wa jinsia katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24.

## **1.1 Suala la utafiti**

Suala la kujamiihana ni swala ambalo limerejelewa na watafiti wengi. Wengi wamelishughulikia Kwa njia tofautitofauti. Ingawa tafiti nyingi zimefanywa kuhusiana na matumizi ya vyombo vya habari, swala la matumizi ya tasfida katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24 halijashughulikiwa, pia hatujui ni aina gani ya tasfida zinazotumiwa, zinatolewa maelezo yapi na zinasawiri nini, licha ya kuwa kipindi hiki hutumia tasfida kinaporejelea maswala ya kujamiihana. Utafiti huu basi unaangazia matumizi ya tasfida hizo, fasiri ya hizo tasfida na jinsi zinavyodhahirisha swala la jinsia katika mawasiliano.

## **1.2 Madhumuni ya Utafiti**

Utafiti huu unadhamiria;

- (i) Kutambua na kueleza tasfida za kijamiihana zinazotumiwa katika Kipindi cha *Connect* cha K24.
- (ii) Kujadili swala la jinsia katika tasfida za kujamiihana zinazotumiwa katika Kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24.

## **1.3 Maswali ya Utafiti**

Utafiti huu unanuia kujibu maswali yafuatayo:

- (i) Ni tasfida zipi za kujamiihana zinazotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24 na zinatolewa maelezo yapi?
- (ii) Swala la jinsia katika tasfida za kujamiihana zinazotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24 linadhihirikaje?

## **1.4 Umuhimu wa Utafiti**

Tumechagua mada hii kwa sababu tasfida ni muhimu sana katika uwanja wa isimu. Kwa hivyo utafiti huu utasaidia uwanja wa isimu hasa pragmatiki na semantiki kwa kuwa ulishughulikia jinsi lugha inavyotumika katika jamii.Utafiti huu utawasaidia wazazi, walimu na hasa wa maswala ya jamii kwa kuwa utawawezesha kuelewa maswala muhimu ya kujenga familia thabitii.Utafiti huu utawasaidia wasomi wa maswala ya kijinsia na watafiti wanaotumia nadharia ya uchangunuzi hakiki usemi.

## **1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu ulihusu kipindi cha runinga ya K24 cha *Connect*, uliangazia matumizi ya tasfida katika kipindi hicho cha *Connect* cha kifamilia, na ulidhamiria kutambua, kufasiri tasfida na kuelezea jinsia tasfida hizo zinavyosawiri swala la jinsia. Utafiti huu unahuishisha tasfida zinazotumika katika kipindi hicho cha *Connect* cha runinga ya K24 pekee na ulishughulikia tasfida zilizotumiwa katika kipindi cha *Connect* kati ya mwaka wa 2011 na 2012.

## **1.6 Maelezo ya Istilahi**

**Connect:** –Jina la kipindi cha runinga kinachofanyiwa utafiti. Kinaitwa *Connect* kwa sababu kinaunganisha watu kutoka sehemu mbalimbali za nchi.

**Jamii:** Kundi la watu maalum wanaotofautiana na makundi mengine kwa misingi ya lugha desturi na mila.

**Jinsia:** Hali ya kuwa kiume au kike. Sifa za uana yaani, kuwa mwanamke au mwanamume.

**Kujamiihana:** Kufanya tendo la ndoa.

**Kuumeni:** Kuegemea upande wa kiume (mwanaume).

**Ukeni:** Kuegemea upande wa kike (mwanamke).

**Mdahalo:** Usemi ambao unaweza kuwa ama umetamkwa au uko katika maandishi.

**Tasfida:** Matumizi ya lugha ya adabu, iliyopunguzwa makali.

**Uwezo :** Ni nguvu au mamlaka aliyonayo mtu au watu katika jamii. Ni tofauti za kiuhusiano na miundo ya kitabaka katika jamii.

## **SURA YA PILI**

### **MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA**

#### **2.1 Utangulizi**

Katika sura hii mtafiti alipitia maandishi yanayohusiana na mada yake ya utafiti na aliiweka katika sehemu mbili kuu, Mapitio ya maandishi na misingi ya nadharia.

#### **2.2 Mapitio ya maandishi**

Sehemu hii ilishughulikia maswala mbalimbali yaliyowekwa katika vichwa vidogo vidogo.

##### **2.2.1 Dhana na Dhima ya Tasfida**

Kamusi ya karne ya ishirini na moja (2011) inatafsiri tasfida kama tamathali ya usemi inayotumia lugha fiche badala ya kutumia lugha ya karaha au matusi. Tasfida hutokana na maneno ambayo ni mwiko katika jamii. Kulingana na kamusi ya karne ya ishirini na moja (2011) mwiko ni jambo ambalo mtu amekatazwa au hawezি kulifanya kutokana na imani, msimamo wake au mazoea. Maneno ya mwiko ni kama vile kutaja kitendo cha kujamiiiana, sehemu za siri, majukumu ya sehemu za siri na huhitaji kutumia tasfida. Katika lugha ya Kiingereza sehemu ya siri ya mwanaume (penis) inaweza kuitwa lollipop, pistol, Aaron's Rod. Katika utafiti wetu tulizingatia tasfida za kujamiiiana zinazotumiwa katika kipindi cha runinga ya K24 cha *Connect*, pia tulionyesha jinsi tasfida hizo zinavyosawiri jinsia.

Locher (2004) anasema kuwa tasfida ni kuepukana na tahayuri na kuonyesha unyenyekevu. Katika maingiliano ni muhali wanaowasiliana kuzingatia sheria ya kuheshimiana na kufikiriana ili kusiwe na kule kufedheheka. Naye Qing (2005) anadai kuwa kupunguza aibu au makali ya maneno hakuwezi kutoka upande mmoja mbali inafaa kutoka katika pande zote mbili yaani wote wanaohusika.

Thomas (1995) naye anasema kuwa kutumia lugha ya mafumbo (indirectness) ni mbinu moja ya kiisimu watu hutumia kuzuia kuzungumzia mada ambazo ni mwiko kama vile kujamiiiana. Mbinu hii hudhamiria kuwa na heshima au adabu katika maingiliano. Brown na Levinson (1987) wanasema kuwa mbinu ya heshima au adabu huzuliwa ili kuzuia kumwaibisha mwingine na kumfanya asikie ametosheka au mtulivu. Vitendo vyta kuaibisha (Face threatening Acts (FTA) ni vitendo ambavyo huasi haki ya msikilizaji na kumfanya asijiheshimu. Mbinu ya adabu husaidia kujitenga na vitendo vyta kuaibisha. Husaidia

wahusika kutulia na ndiposa watu wengi wanaokitazama kipindi cha *Connect* cha K24 huwa hawaabiki kutokana na matumizi ya tasfida na husaidia familia nyingi kupata mafunzo.

Brown na Levinson (1987) wanaendelea kushikilia kuwa heshima (politeness) ina jukumu la kimsingi katika jamii. Inadhibiti ugomvi (migogoro) kati ya wanaowasiliiana. Hata hivyo heshima katika usemi hutathminiwa kulingana na kanuni na maadili yanayofungamana na tamaduni na hutofautiana kutoka utamaduni mmoja hadi mwingine, kumaanisha kuwa mwelekeo wa heshima hutegemea muktadha katika tamaduni mbalimbali kwa hivyo nadharia tunayotumia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi ilikuwa na jukumu kubwa katika utafiti wetu, kwa kuwa tasfida zilichanganuliwa kutoka kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24 nchini Kenya.

Nadel, (2004) linaonyesha jinsi wanaume wa Afrika Magharibi walivyodhahirika kama watu wenye heshima na adabu duniani, kwa kutofautisha baina ya vishazi na istilahi zilizosawa katika mazungumzo ya unyenyekevu na yasiyo ya unyenyekevu. Wao hawazungumzii maswala ya kujamiiiana na sehemu za siri moja kwa moja bali hutumia maneno ya heshima ili kuzuia vikwazo vya mawasiliano. Ingawa Nadel hakuzungumzia jinsia katika utafiti wake, jambo ambalo tulilizingatia alilichangia kwa sababu alishughulikia maswala ya ngono na matumizi ya lugha ya heshima au adabu (tasfida).

Berlin na Kay (1969) nao wameeleza kuwa lugha ya tasfida hutumika ili kuepukana na kutaja mambo ambayo hayawezi kusemwa, sio kwa sababu hayasemeki bali inabidi watu watumie tasfida kuyazungumzia. Wao wanaeleza maswala hayo, lakini katika utafiti wetu tuliyaonyesha,kuyatolea maeleo na kueleza jinsi yanavyosawiri jinsia katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24.Katika maingiliano, wazungumzaji ni lazima wajiheshimu na wajisitiri kutokana na aibu ambayo inaweza kujitokeza. Maneno yanayotumiwa katika mawasiliano ni lazima yawe ya heshima na kumfikiri mwenzako. Si vizuri kuelezea mambo fulani au ukweli fulani moja kwa moja, lakini kwa kutumia tasfida, kutasaidia kuondoa aibu kwa wanaowasiliiana.

Kulingana na Locher (2004) inabidi wazungumzaji wajiepushe na hali ya kuaibisha na wanaozungumziwa kutokuwa watulivu kutokana na haya. Ni jukumu la mzungumzaji kujiheshimu na kuonyesha anaowazungumzia heshima kwa kutumia maneno ya tasfida .Anaendelea kusema kuwa, dhima ya tasfida ni kuepuka fedheha na kuonyesha

unyenyekevu. Katika utafiti wetu tulitarajia kuonyesha jinsi tasfida hizo zinavyodhihirisha tofauti za kijinsia na pia katika uteuzi wa tasfida alizozitumia mwasilishaji.

Meyerhaff (2006) anasema kuwa nadharia ya Brown na Levinson inazingatia uteuzi wa maneno na vifungu vyta maneno vinavyofaa kulingana na miundo ya kijamii. Kutohakana na maoni hayo inaonyesha kuwa tasfida ni uteuzi wa maneno na vifungu vyta maneno mwafaka. Uteuzi mwafaka wa maneno yanayofaa husaidia katika kupunguza aibu kati ya wazungumzaji, hii ni kwa sababu tasfida ni kielelezo cha matumizi ya lugha fiche au lugha isiyo ya moja kwa moja. Lugha ya wazi inaweza kuwa ya aibu lakini fiche, husitiri aibu kati ya mzungumzaji na mzungumziwa hasa watu wanapojadiliana maswala nyeti kama vile kujamiihana kama vile afanyavyo mwasilishaji wa kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24.

Sanderson (1999) anaeleza kuwa tasfida huonyesha uhusiano baina ya lugha ya mwiko na tafsida. Anaendelea kusema kuwa kiini cha tasfida ni maneno ya mwiko. Maneno ya mwiko ni maneno ya aibu na ya kufedhehesha yanapotumiwa katika mawasiliano. Katika utafiti wetu tulizingatia tasfida zilizotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24 na kuzitolea maana ambayo kwa hakika kama istilahi hizo zingetumiwa zilivyo zingekuwa ni mwiko kwa kuwa kweli zinadhahirisha kufedhehesha na zingekwamisha au adhiri mawasiliano kati ya mwasilishaji na mtazamaji.

Zhenqiang (2006) anasema kuwa tasfida ni maeleo yasiyo ya moja kwa moja yanayotumiwa kwa niaba ya maneno makali. Anaendelea kusema kuwa karibu mila zote zina maneno ambayo watu hujaribu kuyahepa kutaja moja kwa moja hata kama kuna maneno hayo katika lugha. Utafiti huu uludhamiria kuangalia tasfida zinazotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24.

Kutumia tasfida kunaonyesha matumizi ya lugha ya unyenyekevu na kulingana na Ambuyo (2011) akitafiti kuhusu adabu katika muktadha wa kisiasa wakati wa maswali katika mjadala wa bunge la Kenya, aliteta kuwa wakati wa maswali ni muhimu na huwa na majibizano mengi hivi kwamba ni rahisi wabunge kutumia lugha ya aibu kwa wenzao. Kutohakana na matumizi ya lugha ya wabunge, kuna sheria ambayo hudhibiti jinsi wanavyotumia lugha bungeni. Sheria hii imesaidia katika kuendeleza mjadala ambaou unazalisha matunda mema. Matokeo ya utafiti wake, yalionyesha jinsi mikakati fulani inavyoweza kutumiwa kuondoa aibu na kufanikisha mawasiliano mema. Utafiti huo wa Ambuyo ni muhimu kwa kuwa ulionyesha kuwa matumizi ya lugha ya adabu (tasfida)

yanarahisisha na kufanikisha mawasiliano. Katika utafiti wetu jambo hili tulilizingatia kwa kuwa tulidhamiria kuonyesha jinsi mwasilishaji aliteua istilahi za tasfida, kuzitolea maana na hata kuigiza katika runinga maswala nyeti ya ndoa.

Tasfida hizi zinazotumika zinadhihirisha uwezo wa kijinsia kwa njia fiche. Mambo haya ndiyo yaliyotuchochea sisi kama watafiti kuchagua kipindi hicho cha *Connect* ili tukifanyie utafiti kuhusu matumizi ya tasfida za kujamiana na usawiri wa jinsia. Tafiti ambazo tayari zimefanya kuhusu vyombo vya habari zikiegemea upande wa lugha si nyingi. Manka (2011) alitafiti kuhusu, Tafsiri ya matangazo ya runinga kuhusu UKIMWI kati ya wanafunzi wa sekondari katika Wilaya ya Njoro na Kaunti ya Nakuru. Ontieri (2005) alitafiti kuhusu uchanganuzi wa matumizi ya lugha katika magazeti ya Kiswahili nchini Kenya, akizingatia gazeti la Taifa Leo. Katika upekuzi wetu hatukuona mtafiti ye yote aliyetafiti kuhusu matumizi ya tasfida za kujamiiiana na usawiri wa jinsia katika chombo chochote cha habari. Ni kutokana na hilo pengo ambapo tuliamua kufanya utafiti wetu katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K 24 nchini Kenya.

### **2.2.2 Lughha, Kujamiiiana na Jinsia.**

Katika jamii nyingi maswala ya kujamiiiana hayazungumziwi hadharani. Kutaja au kuzungumzia maswala haya huwa ni mwiko kama asemavyo Bakhtin (1984) katika Mwanzandi (2001). Huang, na Tian, (1990) wanatafsiri mwiko kuwa kitu ambacho kimekatazwa kutokana na mila na desturi za jamii. Watu wengi huchukulia maneno au mafungu ya maneno ambayo ni mwiko kama lugha chafu, mambo ambayo huhuishwa na kujamiiiana na kutaja sehemu za siri au nyeti za mwili. Ni kutokana na mtazamo huu ambapo mwasilishi wa kipindi cha *Connect* aliamua kutumia lugha fiche ya adabu (tasfida) katika kipindi chake ambacho kinaangaziwa katika utafiti huu.

Kujamiiiana huelekezwa na utamaduni. Watu tofauti huzua hisia zao tofauti za kujitambulisha kijinsia na kuuonea shauku muktadha wao wa wakati maalum katika historia, hadhi yao ya kijamii, kabila lao, dini na mipangilio inayoelekeza majukumu ya kijinsia (Foucault 1978; Rubin 1984). Kila tamaduni ulimwenguni hudhibiti jinsia ya binadamu na ndiposa wanaume wana uwezo wa kijamii na kisiasa na wao ndio hufaidika. Wanawake kutokana na miundo ya kitamaduni ya uana na kujamiiiana huishi maisha ya wasiwasi kati ya raha na hatari (Joseph na Lewis, 1981). Ni kutokana na haya, kipindi hiki kinawalenga sana wanawake. Utafiti kuhusu uhusiano wa lugha na jinsia umekuweko zaidi

ya miaka hamsini, lakini kazi nyingi zilijihuisha na kujamiihana kwa jinsia moja (homosexuality). Tafiti za zamani zilishughulikia kimsingi kuhusu kujielezea kijinsia kupitia maneno fulani ya kipekee (Legman 1941, Cory 1951 na Rodgers 1972)

Kuanzia mwaka wa 1980 mwelekeo ulibadilika kutoka kuangalia jinsi jinsia au kujamiihana kunavyoonyeshwa katika lugha kuelekea majoribio ya vile kujamiihana/jinsia inavyoundwa kimaelezo kupitia lugha kwa mfano, Hall na Bucholtz (1995), Leap (1995, 1996). Leap anasema ni muhimu kushughulikia lugha na jinsia kwa sababu kujamiihana hakuwezi kuelezewa kwa kurejelea jinsia pekee. Swala la usomi wa jinsia ni makisio ya uwezo na jinsi maswala hayo hutekelezwa na kusambazwa. Kujamiihana ni usomi wa jinsi watu huvuka mpaka (kosea), hulazimisha na kufanya kazi kwa kuzingatia makisio. Baadaye utafiti wa lugha na jinsia (kujamiihana) ulifanywa kupitia Nadharia ya Queer na ufeministi (Livia na Hall 1997). Bucholtz na Halls (2004) wanaelezea jinsi nadharia hizo (Queer na ufeministi) zilivyoza mwelekeo muhimu katika usomi wa uhusiano wa uwezo unaozunguka kujamiihana na uana au jinsia. Wanabisha kuwa uwezo ni sehemu muhimu ya utamaduni na utamaduni wenyewe unapangiliwa na uhusiano wa uwezo. Utafiti wa Butler (1990) wa ‘gender performativity’ umesaidia sana katika utafiti wa miaka ya karibuni. Livia na Hall (1997) walichukua nadharia ya ‘gender performativity’ ya Butler na kuirudisha nyuma katika mzizi wa isimu wakitumia kazi ya vitendo nenii ya Austin (1962) ya kusema kitu ni kufanya kitu, kwa hivyo tunafanya kitendo kwa kutoa tamko. Kitendo nenii kinayumbayumba, kitendo chenyewe hakitoi maana, lakini maana hupatikana katika maingiliano baina ya kitendo (matini) na muktadha.

Kwa hivyo kujamiihana hakuwezi kuwa kwa sababu ya kuongea na kutenda lakini katika mfanyiko wa kuingiliana baina ya kitendo nenii na tamaduni asilia za kijamii na muktadha wa hali ambapo umetolewa na kupokelewa. Hii ndio Hall (2004), Leap na Boellstorff (2004) wanasisitiza uzingativu mwingi katika muktadha maalum wa maingiliano katika usemi wa lugha, usemi na kujamiihana. Katika utafiti huu swala la muktadha ni muhimu sana ili kuelewa tasfida zilizotumiwa, jambo ambalo mtarufi anakubaliana na watafiti waliotajwa hapo juu. Kazi zinazoangazia maswala mbalimbali ya uhusiano kati ya lugha na kujamiihana zimezuka na kuendelezwa katika nyanja mbalimbali za usemi kama vile uana, sosholojia, anthropopolobia, vyombo vya habari, nadharia ya jamii na utamaduni.

Utafiti huu ulijikita katika chombo cha habari ambacho ni runinga ya K24 ambacho huwafikia watu wengi nchini Kenya na hata nchi za nje. Kulingana ripoti ya shirika la Afya

ulimwenguni (WHO) (2005) Uana ni jambo mtikati katika maisha ya binadamu. Wanasema uana hudhihirika katika fikira, shauku, imani, tabia nzuri, mienendo, dhima na uhusiano. Wanaendelea kusema kuwa uana huathiriwa na maingiliano ya kibayolojia, kisaikolojia, kijamii, kiuchumi, kisiasa, kitamaduni, kikabila, kisheria, kihistoria, kidini na kiroho. Utamaduni wa kijamii huangazia kuathiriwa na desturi za kijamii, ikiwemo vyombo vya habari kama vile siasa na mawasiliano ya umma, vyombo hivi vya habari vinaweza kuleta mabadiliko mengi katika desturi za kijamii. Kipindi cha *Connect* ambacho kinafanyiwa utafiti kimesababisha mabadiliko mengi ya desturi za kijamii hasa Kenya ambapo hairuhusiwi kuzungumza maswala ya kujamiihana hadharani.

Foucault (1989) anadokeza kuwa karne ya kumi na tisa sio wakati ambapo kijamiihana kungenyamazishwa na kuzuiliwa kama ilivyofikirika. Anasema kuwa huo ni wakati ambapo watu walitiliwa nguvu kuzungumzia zaidi kuhusu kujamiihana lakini kwa njia hasi. Alisema ulikuwa wakati wa kuchochea usemi yaani walishawishiwa kuongea. Wakati ambapo kujamiihana (jinsia) ilipangiliwa upya kupitia maongezi haya kuelekea mfumo mpya wa uhusiano wa uwezo. Utafiti huu ulihuisha usemi wa kujamiihana lakini katika mwelekeo chanya ambaeo unadhamiria kuimarisha familia kupitia. Foucault akishughulikia jinsi uana na mwili vimekuwa vielelezo vya uwezo na siasa katika jamii ya magharibi aliangazia jinsi lugha ilivytumiwa na wasomi kukataa uana. Akahitimisha kwa kusema kuwa wasomi hujichagua kama wapatanishi wa kile ambacho ni sawa na si sawa katika uana. Anaendelea kusema kuwa maana ya kijinsia au kujamiihana huwa muundo wa kijamii na kitamaduni na inaweza kubadilishwa kwa kuingilia kati jamii na utamaduni. Swala hili lilielekea kuwa kichochesi kikuu cha kumfanya mwasilishaji kuingilia kati kwa kutoa mafunzo akitumia tasfida.

Wanasosholojia wengi huona kujamiihana (jinsia) kama kielelezo cha muundo wa lugha katika mpangilio wa uhusiano wa uwezo. Wanasosholojia hujihusisha na kuona jinsi lugha huelekeza jinsi tunavyoona kujamiihana. Mwelekeo wa lugha kwa kujamiihana unaweza kwa mfano, kuangalia jinsi watu wanavyoongea kuhusu kujamiihana katika runinga kwa mfano, Oprah na jinsi inavyoathiri jamii nzima. Utafiti wa Foucault (1979) ‘The History of Sexuality’ unadokeza jinsi watu wanavyoathiriwa na kujamiihana. Kusikiliza kipindi hiki cha *Connect* na bibi na bwana kuwa wazi mmoja kwa mwingine na kufurahia maisha yao ya kujamiihana.

Cameron na Kulick (2003) wanatuelekeza jinsi njia ya usemi wa lugha hutumika kuongea kuhusu kujamiihana, jinsi inavyounda maoni yetu kuhusu kujamiihana na kudai kuwa kwa miongo vilevile tumetoka kuona kujamiihana kama tu tabia fulani na kuona kuwa ni sawa au si sawa na kutokana na hayo kumtafsiri mtu kulingana na tabia fulani ya kujamiihana. Kutokana na mwelekeo huu utafiti huu uliangazia mienendo au tabia ambazo hazikubaliki na ambazo zinasababisha kuzuka kwa migogoro kati ya familia. Ndiposa mwasilishaji anajaribu kutumia tasfida ili kutoa elimu kuhusiana na maswala nyeti ya familia. Wanaendelea kubisha kuwa usomi kuhusu kujamiihana lazima uzingatie matumizi mbalimbali ya lugha. Wanasema kuwa kile tunachoju na kuamini kuhusu kujamiihana ni sehemu ya mzigo tunaouleta katika kujamiihana na ujuzi wetu na hautokani na tajriba ya kwanza, inaingiliwa kati na matini zinazozunguka katika jamii. Lugha huzalisha jinsi tunavyosabikia jambo kulitambua na desturi za kujamiihana. Lugha pia huadilisha nafasi na ujuzi wa mada hii ya kujamiihana ikihusisha kiwango cha maingiliano.

Kulingana na *Joint United Nations Programme on HIV/AIDS (UNAIDS)* (2000) watu wengi huona vigumu wakati wa kuzungumzia kuhusu kujamiihana na maswala ya ngono, ikiwa ni kujibu maswali kuhusu kujamiihana kutoka kwa watoto wao, kuongea na wachumba wao kuhusu maswala ya kujamiihana au kuuliza madaktari wao maswali ya kujamiihana. Lakini kunyamaza, hufanya watu kubaki bila kuja na mwishowe kusababisha matokeo mabaya ya uhusiano wa kujamiihana. Wanaendelea kusema kuwa kuachilia watu kuendeleza hadithi za kujamiihana ambazo huwa za uongo na ingawa huonekana kuwa sawa kutokana na kutokuwa na ukweli na uwazi katika mawasiliano ya kujamiihana. Wanaendelea kusema kuwa kwa bahati mbaya kwa kutokuwa na elimu mwafaka ya kujamiihana inamaanisha watu wengi hawana habari hata ya msingi na hii husababisha kizingiti katika mawasiliano mema ya kujamiihana. Ni vigumu kuanzisha mazungumzo kuhusu kujamiihana wakati watu hawana muktadha unaofaa ili kuyaanzisha.

Kutokuwa na habari hata ya kimsingi kuhusu kujamiihana hufanya hata kuongea kuhusu kujamiihana jambo la kuogofya. Utafiti huu ulidhamiria kuonyesha kwamba watu wengi hawana habari yoyote kuhusu kujamiihana. Hii ni kwa sababu wazazi wamekwepa majukumu yao, ya kuwafunza watoto na kuwaachia walimu na watu wa rika lao, jambo ambalo limekuwa shida kubwa. Kwa hivyo kwa kutumia tasfida mwasilishi anajaribu kutoa mafunzo ambayo ni ya manufaa makubwa katika familia mbalimbali nchini Kenya na hata nchi zingine za nje. Naye Adei(1991) anaeleza kuwa watu wachanga katika ndoa hasa bibi

harusi huona vigumu kuzungumzia swala la kujamiiiana na waume wao. Hata huona vigumu kuvua nguo zao mbele za waume wao hasa siku za kwanza kwanza za ndoa yao. Haya ni matokeo ya mafunzo ya maadili katika jamii. Anaendelea kusema kuwa jambo ndogo kuhusu kujamiiiana katika familia linaweza kusababisha mgogoro katika familia na lazima lishughulikiwe kwa uangalifu sana.

Christensen na Miller (2006) nao wanasema kuwa kujamiiiana ni shida ya kawaida katika ndoa na huhusisha mambo mengi yanayohusiana na mtagusano wa kujamiiiana kama vile kujamiiiana na mara kwa mara tofauti za kihisia, kiwango au thamani ya ngono na ngono ya kuzini. Shida nyingi za kifamilia hasa kuhusu kujamiiiana zimesababisha kutalakiana kwa familia nyingi na kutokana na kipindi kinachotafitiwa cha ‘*Connect*’ usaidizi umepatikana ambapo familia nyingi zilizolekea kutalakiana zimepata mafunzo na kutulia.

Kulingana na utafiti wa Onyango (2011) mwanamke katika jamii nyingi za Kenya anatarajiwa kujikakamua ili amfurahishe mumewe kingono na inadaiwa kuwa asipofanya hivyo anampa mumewe kibali cha kutafuta wanawake wengine. Anaendelea kusema katika baadhi ya jamii za Magharibi mwa Kenya walioingiliana na Waganda mwanamke ni lazima ang’ang’anie kumvutia mumewe kingono ili aweze kumsitiri dhidi ya wanawake wengine kutoka Uganda wanaoweza kumvutia.

Mwanamke asiyemtosheleza mumewe kingono huonekana kana kwamba ni bure. Mwanamke ana majukumu mengi kama vile, kulima, kuchota maji, kutafuta kuni, kupika, mlezi na zaidi kumfurahisha mumewe kingono. Katika kipindi cha *Connect* mwasilishi anajaribu kuwafunza wanawake jinsi ya kutekeleza majukumu hayo yote bila kuwasahau waume bado wanawasubiri. Mafunzo haya anayapitisha kwa kutumia tasfida.

Naye Benjamin katika jarida lake la lugha na kujamiiiana analenga kuwasilisha utafiti kuhusu uundajielezi wa ashiki, utambuzi, siasa na uana (kujamiiiana) nchi za nje akilenga kazi katika isimu. Kwa mawanda mapana iwezekanavyo pamoja na uchanganuzi isimu tendakazi, isimu anthropolojia, pragmatiki, semantiki, uchanganuzi matini na kanuni zingine za lugha kupitia maswali ambayo yatachangia utafiti wa matini za uana au kujamiiiana na matokeo ya kiisimu na kijamii.

Greer (2000) akizungumzia kuhusu jinsia anasema kuwa swala la kuegemea kuume limekita mizizi katika utamaduni na jamii, na ni gumi sana kuliondoa. Anadokeza kuendelezwa kwa kuegemea kuume katika sehemu mbalimbali: Kwanza, katika kujamiiiana

ni mwanamume ambaye amepata uhuru akilinganishwa na mwanamke, lazima mwanamke amtosheleze mwanamume kingono, lakini swala na mwanamke kutoshelezwa limepuuzwa. Pili, mwanamke bado anatarajiwa aushughulikie mwili wake na jinsi anavyoonekana. Hajaruhusiwa avalie na aonekane apendavyo bali amewekewa vikwazo. Tat, mwanamke bado anamwogopa mwanaume. Swala la mwanamume kuonekana mwenye uwezo linatiliwa mkazo na wanaowafunza wanawake wawaogope wanaume visirani kama vile wabakaji. Greer anaendelea kusema kuwa wasichana wanafunzwa sheria za kuwa wanawake tangu utotoni na ndiposa wanakuwa na haya kuhusu miili yao na kupoteza uhalisia wao na haki ya kujitawala. Matokeo yake huwa ni udhaifu, kujitenga, kujidunisha na kukosa furaha. Greer anabisha kuwa wanawake wanatakiwa kujua na kukubali miili yao na kuachana na hali ya useja.

Connel (2011) naye anaeleza kuwa jinsia ni namna mienendo ya kijamii inavyopangwa. Mienendo hii huhuishwa na mikakati ya kuzaa na miundo ya mwili wa binadamu. Mienendo ya kijinsia haijafungamanishwa na matendo tengwa bali tawi la mkusanyiko wa mienendo ya kijinsia. Connel anaeleza kuwa jinsi taasisi zilivyopangiliwa kijinsia sio tu kijazanda bali kwa namna inayodhihirika au utendaji. Anatoa mfano wa nchi ilivyopangwa kijinsia kwa mpangilio wa mienendo kwa kuhusisha uwanja wa uzalishaji, kwa ukweli kuwa wanaume ndio bado wanashikilia nafasi zenye uwezo katika nchi sio sababu ya kipekee kuwa nchi inaegemea kuume bali ni matokeo yake. Anabisha kuwa uume hujumuisha taratibu mbalimbali na mwishowe hufikia mitafaruku ya ndani na mabadiliko ya kihistoria. Ili kutambua jinsia kama ruwaza ya kijamii ni lazima ionekane kama tukio la kiihistoria na linalozua historia. Hii ndio sababu swala la jinsia linajitokeza waziwazi katika matumizi ya tasfida katika kipindi cha *Connect*.

Nchini Kenya wasomi wengi wametafiti swala la lugha na jinsia wakiwemo Aswani na wengine (2006) ambao wanadai kuwa mabadiliko ya kiisimujamii hutegemea jinsia. Wanabisha kuwa mazungumzo baina ya wanawake na wanaume hutofautiana kimaumbo, kimada, kimaudhui na kimamatamshi. Wanaume hupenda kuonyesha uwezo na hili ndilo mwasilishi wa kipindi cha runinga ya K24 cha *Connect* anaonyesha kwa kutumia tasfida ambazo zinamtukuza mwanaume. Katika utafiti wetu tulionyesha jinsi tasfida zilizotumiwa katika kipindi cha *Connect* zinavyodhihirisha uwezo wa mwanamume dhidi ya mwanamke katika jamii: David (2006) katika utafiti wake anaonyesha jinsi wanawake wamesawiriwa katika lugha ya Ekegusii kwa kuzingatia methali hivi kwamba wanaume wametukuzwa

ilhali wanawake wametwezwa. Abudi (2011) alionyesha jinsi wanawake wanavyodunishwa kupidia lugha, kwa kuzingatia lugha Dholuo kwa misingi ya jazanda na misemo. Katika utafiti wetu tuliangazia jinsi jinsia imesawiriwa katika matumizi ya tasfida katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24.

Tofauti za kijinsia hudhihirika kwa msingi wa bayolojia ilhali dhima ya kijamii hudhihirika kwa misingi ya kitamaduni. Usawiri wa kijinsia hudhihirika kupidia lugha. Katika utafiti wetu tulizingatia istilahi za tasfida za kujamiihana katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24. Tulizingatia jinsi mwasilishaji alitumia lugha ya tasfida katika uteuzi wake wa istilahi za kujamiihana katika kipindi hicho. Tulizingatia maelezo yaliyotolewa tasfida hizo na jinsi tasfida hizo zilisawiri jinsia.

Nelson (1990) katika Ndambuki (2010) anasema kuwa wanawake hulinganishwa na majukumu yasiyoepukika kama vile: kupata hedhi na kupachikwa mimba, ilhali wanaume hulinganishwa na majukumu yanayohitaji nguvu za mwili. Katika Kiingereza mwanamke husawiriwa kama kiumbe cha kukaa tu (passive) na mwanamume kiumbe tendaji(active). Kiingereza pia kinamsawiri mwanamke kama kitu cha kula na kulinganishwa na mimea kama vile sweet(peremende) na kuvunja ubikira (deflowering). Utafiti huu wa Nelson ulitusaidia katika utafiti huu wetu kwa sababu ulielezea majukumu ya wanawake na wanaume na tuligundua kuwa uteuzi wa tasfida alizozitumia mwasilishaji wa kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24 zingine zinarejelea majukumu fulani katika jamii. Utafiti wetu ulijikita katika matumizi ya lugha ya tasfida za kujamiihana na usawiri wa jinsia katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24 ilhali Nelson katika lugha ya Kiingereza.

Choti (1998) katika "Lugha na mfumo wa ngazi katika lugha ya Kikisii" anadhihirisha jinsi viambajengo vya Kiisumu humsawiri mwanamke. Utafiti wake unadhihirisha kuwa mwanamume husawiriwa kama binadamu mwenye uwezo tofauti kabisa na mwanamke ambaye, jamii humsawiri kwa njia hasi, tofauti na mwanamume. Mawazo hayo ya Choti yalitufaidi katika utafiti wetu kwa sababu tulizingatia jinsi jinsia inavyosawiriwa katika tasfida za kujamiihana alizozitumia mwasilishaji wa kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24.

Riro (2006) katika utafiti wake kuhusu Usawiri wa mwanamume katika nyiso za jando za Abakuria, anabainisha jinsi matarajio, mitazamo na mielekeo ya jamii huchukua nafasi

kubwa katika kuratibu majukumu kiuana na kutathmini thamani ya kila jinsia. Riro amedhihirisha kuwa jamii ya Abakuria humsawiri mwanamume kwa njia chanya tofauti na mwanamke. Nyiso za jando za Abakuria hudhihirisha uwezo mkubwa alionao mwanamume katika nyanja mbalimbali katika jamii. Kwa mfano, katika sheria, siasa, utawala, uchumi na mamlaka juu ya maamuzi na maafikiano katika jamii. Utafiti wa Riro umekitwa katika utanze wa Fasihi simulizi ya Wakuria na pia umeangazia jinsia ya kiume kwa upekee wake. Utafiti wetu ulilenga swala la jinsia kijumla, jinsi linavyosawiriwa katika matumizi ya tasfida za kujamiana katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24.

### **2.2.3 Mawasiliano ya Runinga**

Mawasiliano ni upashanaji wa habari kwa kutumia barua, simu au vyombo vya habari kama vile redio, televisheni na kadhalika. Mawasiliano kuitia vyombo vya habari ni muhimu katika maisha ya kisasa na hutekeleza dhima kubwa katika kuelekeza namna tunavyotumia wakati wetu na jinsi tunavyoishi (Baran, mctyne na meyer (1984). Ni muhimu kutambua kuwa tunaishi katika mazingira ambayo yana wingi wa vyombo vya habari ambavyo hutuathiri moja kwa moja katika maisha yetu ya kila siku. Jinsi tunavyoishi hatuwezi kuendelea bila kutumia vyombo vya habari vya umma na jinsi teknolojia inavyopenya kila sehemu ya nchi, maisha ya baadaye yanatarajiwa kutegemea vyombo vya habari. Kutokana na utafiti wa Baran inasemekana kuwa asilimia sitini na nane ya familia za Marekani wana runinga na huwa inatumika kwa kadri ya masaa sita na nusu kila siku. Ni muhimu kutaja hapa kuwa kutokana na maendeleo ya kiteknolojia watu wengi hutumia runinga.

Runinga au televisheni ni chombo ambacho hunasa picha, sauti na maandishi kutoka kituo kimoja cha mawasiliano na kuziwasilisha kwa watazamaji katika sehemu nyingine (kamusi ya karne ya 21: 2011: 494). Majaribio ya utangazaji kwa kutumia runinga yalianzishwa mwaka wa 1920 kule Amerika na Bara la Uropa majaribio haya yalitumia ‘Mechanical scanning disc’ ambayo haikuonyesha picha vilivyo. Kufikia mwaka wa 1923 kulivumbuliwa ‘Iconoscope’ the electric television tube. Uvumbuzi wa ‘Kinescope’ au neli (tube) ya picha, kamera ya kielektroniki na kipokezi cha televisheni nyumbani uliendeleza kukua kwa runinga. Kufikia mwaka wa 1930 shirika la ‘National Broadcasting Corporation’. Lilikuwa limeanzisha stesheni ya Runinga kule Newyork na BBC stesheni ya televisheni kule London na kuonyesha vipindi mbalimbali. Pia Ujerumani na Ufaransa zilianzisha stesheni za Televisheni.

Kufikia mwishoni mwa 1940 na mwanzoni mwa 1950 televisheni ilikuwa imesambaa nchi zote ambazo zimeendelea. Kufikia mwaka wa 1948 kulikuwa na zaidi ya stesheni arobaini na moja ambazo zilikuwa zikitazamwa katika miji ishirini na mitatu. Katika muda wa miaka kumi (mwongo) stesheni zilikuwa zimeongezeka kutoka 533 hadi milioni Hamsini na tano. Uvumbuzi wa setlaiti ya mawasiliano (1962) ulisaidia kuenea zaidi kwa stesheni za runinga. Leo kila nchi imeunganishwa na setlaiti na wanaona runinga. Uvumbuzi wa tarakilishi na Japan ulisaidia zaidi ukuaji wa stesheni za runinga. (Kumar, 2005) Leo hii runinga ndiyo mojawapo ya njia za mawasiliano duniani kote Nchini Kenya watu wengi wana runinga hasa wale wanaoishi mijini. Watu wengi hutazama vipindi mbalimbali, video na husaidia sana kujua yale yanayoendelea na kujua mbinu mpya za mawasiliano. Televisheni husaidia pia katika kujiburudisha na ni vyema kutazama vipindi vifaavyo katika runinga.

Kuna vipindi ambavyo huendeleza vita na mienendo mibovu na ni vizuri watazamaji kujiepusha navyo kwa kuwa si lazima vitazamwe. Kutokana na wingi na kuwepo kwa televisheni utafiti wa kisasa unaonyesha kuwa ina umuhimu mwingi na inahitaji utafiti katika vipindi vinavyowasilishwa na hii ndio sababu kama watafiti tuliamua kutafiti kipindi cha *Connect* cha K24.

Larsen (1968) anasema kuwa ni kweli kuwa vyombo vya habari kama vile runinga huathiri watazamaji kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja. Anatoa mfano wa mtoto kuathirika kihisia anapotazama vipindi mbalimbali na matokeo huwa anapata jinsi ya kujikinga msisimiko, uchovu na ndoto, Anaendelea kusema kuwa anapoendelea kutazama runinga kwa muda mrefu sana anaweza kujifunza misamiati habari tofauti na imani ambayo inaweza kumtia nguvu au kudhoofisha tabia zake. Tuliangazia athari za matumizi ya tasfida katika *Connect* cha K24,kwa watazamaji. Athari hizo zinaweza kuwa hasi au chanya. Crystal (1992) anasema kuwa vyombo vya habari hutumika katika jamii kujiburudisha na kuitisha ujumbe kwa watu. Dhamira kuu ya Kipindi cha *Connect* cha K24 ni kuelimisha yaani kuitisha vjumbe kwa familia, kwa hivyo mtafiti anakubaliana na maoni ya Crystal ya kuwa vyombo vya habari hupitisha ujumbe na kuelimisha watu kuhusiana na maswala mbalimbali.

Kuna vipindi vingi vya runinga ambavyo huangazia maswala ya kujamiihana, kwa mfano kuna ‘True blood’ mad men’ ‘True word’, Tudors,Buffy the vampire slayer,six feet under,Nick Tuck,American,Horror story came of Thrones,The scandal, New Girl Oprah na

kadhalika. Vipindi hivi vyote huangazia uzuri na ubaya wa kujamiana na watu wengi ulimwenguni hujifunza mengi kutoka kwa vipindi hivi.

## **2.3 Misingi ya Nadharia**

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi (UHU). Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi ilitokana na isimu hakiki ambayo ilizuka katika Chuo Kikuu cha Angalia Mashariki katika mwaka wa 1970. Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi (UHU) ilianzishwa kama ruwaza ya wasomi mwanzoni mwa 1991 kutokana na warsha huko Amsterdam, January 1991. Kutokana na mchango wa wataalam wafuatao, Teun Van Dijk, Norman Fairclough, Gunther kress, Theo van Leeuwen na Ruth Wodak waliochukua muda wa siku mbili kujadiliana nadharia na mbinu za utafiti wa uchanganuzi matini na hasa Uchanganuzi Hakiki Usemi. Mwanzo huu wa ruwaza ya uchanganuzi hakiki usemi, ulitiwa nguvu kwa kuanzishwa kwa majarida ya ‘Discourse and Society (1990)’ na Van Dijk, Language power and ideology (1989) na Ruth Wodak, Language and power (1989)na Norman Fairclough, Prejudice in Discourse (1984) na Teun Van Dijk. Mkutano huu wa Amsterdam ulianzisha taasisi iliyozishwa masomo ya kubadilishana (ERASMUS) kwa miaka mitatu miradi mingi ya pamoja na uhusiano ilianzishwa kati ya wataalam mbalimbali na mielekeo pamoja na maswali spesheli ya usemi na jamii ambayo ililetu mielekeo tofauti ya wataalam mbalimbali pamoja.

Uchanganuzi Hakiki Usemi kwa mara ya kwanza ilianzishwa na shule ya Lancaster ambamo Norman Fairclough alikuwa mtu mashuhuri. Pia Ruth Wodak amechangia sana katika uwanja huu. Msingi wa nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi ni kuwa lugha ni shughuli ya kijamii (Fairclough na wodak 1997) na huchukulia matumizi ya lugha kimuktadha kuwa muhimu (Wodak 2000c) Uchanganuzi Hakiki Usemi (UHU) hutilia maanani uhusiano kati ya lugha na uwezo. Kiambajengo msingi cha uchanganuzi ni matini au usemi kwani, ndicho kipashio muhimu cha mawasiliano. Nadharia ya Uttu huchanganua muundo uliowazi na usiwazi wa mahusiano ya kimamlaka, kiubaguzi, kiuwezo na kiutowala ambayo hudhihirisha na lugha.

Nadharia hii imetafsiriwa na wataalam wengi, Schiffri (1987) anasema uchanganuzi usemi ni jaribio la kuchunguza mpangilio wa vipashio vya lugha ambavyo ni vikubwa kuliko sentensi na kirai. Anaendelea kusema kuwa UHU hushughulikia matumizi ya lugha katika miktadha ya kijamii.

Brown & Yule (1993) wanasema Uchanganuzi Hakiki Usemi (UHU) ni uchanganuzi wa lugha katika uamilifu wake, wanaendelea kusema kuwa hivyo basi uchanganuzi huu

hauwezi kuwekewa mipaka ya kiisimu na ni lazima uchunguzwe kwa misingi ya matumizi yake katika miktadha mbalimbali kutegemea watumiaji. Kress (1985) alidhihirisha jinsi nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi(UHU) ilikuwa ya kipekee katika kuchanganua lugha. Alisema kuwa:

- (a) Lugha ni swala la kijamii.
- (b) Makundi ya kijamii taasisi za kijamii na kila mwanajamii huwa na maana halisi na thamani ambazo hubainishwa kupitia kwa lugha katika mawasiliano.
- (c) Matini na usemini viambajengo mwafaka vya lugha katika mawasiliano.
- (d) Wasomi na wasikilizaji si wapokezi tu bali wanahusiana na matini.
- (e) Kuna uhusiano kati ya lugha ya kisayansi na lugha ya taasisi au jamii.

Kutokana na makisio haya uamilifu wa lugha ulibainika sio tu kwa mawasiliano bali huhifadhi itikadi, mielekeo na matarajio ya watumizi wake. Stubbs (1983) anasema usemi huhusisha majoribio ya kutafiti si mpangilio wa lugha zaidi ya sentensi au virai, kwa hivyo hutafiti viambajengo vikubwa vya isimu kama vile mazungumzo au matini zilizoandikwa. Hili ni dhihirisho kuwa uchanganuzi usemi hujuhusisha na lugha inayotumiwa katika muktadha wa kijamii hasa katika maingiliano na mazungumzo. Kipindi cha *Connect* K24 huunda muktadha mwema ambao huuliza maswali na kujibiwa na pia mafunzo hutolewa.

Fairclough (1989) anabainisha mikakati maalum ya kuchanganua lugha kutokana na uhusiano wa uwezo, itikadi na mabadiliko ya kijamii na utamaduni. Utafiti wake ulizingatia vyombo vya habari na uliangazia uwezo na mapambano kama lugha ni ya wazi. Anadai kuwa taasisi nyingi za vyombo vya habari huwa na ubaguzi na huzua usemi kwa umma na kusema eti wanapeana maoni na tetesi za wanahabari. Fairclough (1995) anasema kuwa itikadi na mamlaka hudhihirika na hutolewa katika matumizi wa kila siku ya mazungumzo na matini amzo huonekana kuwa za kawaida na zilizokumbalika kutokana na maoni haya ya Fairclough utafiti huu uliangazia tasfida za kujamiihana zianazotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24 ili kuchunguza kama zinasawiri jinsia au la.

Wodak (1996) anashikilia kuwa lugha ni tendo la kijamii na anasisitiza muktadha wa matumizi ya lugha ni muhimu. Anaendelea kusema kuwa usemi ni zao la mtu mmoja na huongozwa na tofauti za kimamlaka ambazo ni sehemu za jamii. sifa muhimu ya mtazamo huu wa nadharia ya uchanganuzi hakiki usemi ni kule kujihusisha na nadharia hii huwezesha kung'amua na kuchanganua iwapo lugha inayotumiwa katika jamii hujenga,

husawiri au hudumisha ruwaza za kiuwezo katika jamii. Mawazo haya yanafikiana na madhumuni ya utafiti kwa kuwa yaliangazia matumizi ya tasfida katika kusawiri jinsia. Uchanganuzi hakiki katika usemi hutambua umuhimu wa matumizi ya lugha katika muktadha wa kijamii na hubainishwa wazi utendakazi wa itikadi zinazowakilishwa kupitia lugha (Fowler 1991).

Nadharia hii ya Uchanganuzi Hakiki Usemi hulenga matumizi halisi ya lugha na utaratibu wa utangamano wa kijamii kwa hali na muktadha mahsus. Taratibu hizi hubainisha kategoria za kijamii kwa misingi ya mahusiano yao. Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi inadokeza kuwa mjadala na jamii hutegemeana na hujengana. Inaendelea kueleza kuwa usemi hufungamana na muktada wa kihistoria. Hii inamaanisha kuwa usemi hautolewi bila mukthadha na pia usemi hauwezi kueleweka bila kutilia maanani mukthadha wa kitamaduni. Usemi pia hufanya kazi na itikadi. Nadharia hii ya Uchanganuzi Hakiki Usemi ina mihimili mitatu

- (i) Uhakiki
- (ii) Itikadi
- (iii) Uwezo

Uhakiki inamaanisha kuangalia usemi au matini kwa jicho la upekuzi na kuweka hali zote pasi kuegemea upande wowote. Uhakiki pia inamaanisha mtafiti ajitenge na data, data huwekwa katika muktadha wa kijamii na data iambatinishwe na mihimili mikuu ya nadharia (Wodak, 2001) Max Horkheimer aliyekuwa msimamizi wa taasisi ya utafiti wa kijamii cha Frankfurt mwaka wa 1930, ni muhimu sana katika kuzungumzia swala la uhakiki. Alisema uhakiki ni muhimu katika kuendeleza ukombozi wa kikundi ambacho kinadhulumiwa. Alisema pia hakuna mbinu moja ya utafiti ambayo itatoa matokeo ya mwisho na ya kuaminika katika swalii na akasema kuchukua mwelekeo mmoja wa swalii mahsus kuna hatari ya kupata picha potovu. Kwa hivyo alishauri mbinu kadhaa za maswali zitumike ili zisaidiane. Kutokana na maelezo haya ni dhihirisho kuwa uhakiki hupatikana katika kiwango cha mbinu za utafiti.

Itikadi ni mawazo pendwa katika kipindi maalum na huendelezwa katika ishara za namna kwa namna katika jamii. Itikadi ni jinsi fulani ya kuwakilisha na kupanga jamii inayotoa mahusiano yasiyo sawa ya mamlaka, udhibiti na ukandamizaji. Katika mipaka ya Uchanganuzi Hakiki Usemi itikadi inachunguliwa kama hali zinazoibua na kudumisha

mahusiano yasiyo sawa ya kimamlaka. Tofauti katika makundi ya kijamii na itikadi zao zinatokana na mahusiano ya kimamlaka ambayo huzalishwa na kuhalalishwa katika kiwango cha itikadi na maana ili kudhibiti watu wengine.

Thompson (1990) akielezea dhana ya itikadi na utamaduni akihusisha vyombo vyaa mawasiliiano anaashiria kuwa dhana itikadi iliokea mara ya kwanza mwishoni mwa karne ya kumi na nane kule Ufaransa. Anasema imekuwa ikitumika kwa karne mbili na imepewa maana na matumizi mbalimbali katika muda tofauti. Thompson anasema itikadi ni miundo na mifanyiko ya kijamii ambayo kwayo miundo ya ishara huenezwa katika jamii ya ulimwengu. Kulingana na Uchanganuzi Hakiki Usemi (UHU), itikadi ni muhimu katika kuweka na kuendeleza uhusiano wa uwezo usio sawa. Kulingana na Thompson (1990) uchunguzi wa itikadi ni uchunguzi wa njia ambazo kwazo maana huundwa na kupitishwa kwa miundo ya ishara za aina mbalimbali. Lazima uchunguzi huu ushughulikie muktadha ya kijamii ambayo miundo ishara hizo hutumika. Kulingana na Eagleton (1994) uchunguzi wa itikadi lazima uangazie nadharia na wana nadharia kadhaa ambao wameangalia uhusiano kati ya uhalsia wa fikra na jamii. Nadharia zote zichukulie kuwa kuna sababu za kihistoria zinazowafanya watu kufikiria, kuhisi, kushauku na kukisi waonavyo.

Uwezo ni tofauti za kiuhusiano na hasa tofauti katika miundo ya kijamii. Luga ni muhimu sana kuonyesha uwezo hubainisha uwezo wa miundo ya kitabaka katika jamii. Uchanganuzi Hakiki Usemi (UHU) huangazia njia ambazo miundo ya kiisimu hutumika katika kuijieleza na kushurutisha kwa kutumia uwezo unaoweza kujitekeza katika maneno yanayotumiwa na udhibiti katika jamii. Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi huangazia uwezo au mamlaka kwa kuchunguza jinsi jinsia inavyoundwa ikihusishwa na thamani zisizolingana. Katika muktadha wa luga, Uchanganuzi Hakiki Usemi hujihuisha na kuchanganua luga ya walio na mamlaka ambao wanawajibika kwa kutokuwepo na usawa na wale walio na namnana nafasi ya kuboresha hali hizo.

Wodak anasema yafuatayo kuhusu luga na uwezo

- (i) Uwezo ni tofauti katika uhusiano hasa uhusiano wa miundo ya kijamii.
- (ii) Luga siku zote huingiliana na uwezo wa kijamii katika hali mbali mbali.
- (iii) Luga hutoa muhuri kwa uwezo.
- (iv) Luga hueleza uwezo.
- (v) Luga hushiriki katika uwezo.

(vi) Lugha hutumika kупinga uwezo.

Lugha iliyotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha runinga K24 ilidhihirisha uwezo hasa katika matumizi ya tasfida na kufanya wasikilizaji wengi kushabikia kipindi hiki ambacho kina mafunzo mazuri sana.Uchanganuzi hakiki katika vyombo vyahabari umeangaziwa na Wood (1983;1) ambaye anasisitiza kuwa utafiti wa vyombo vyahabari ufanywe. Anasisitiza kuwa itakuwa bora zaidi ukijua mengi yanayowasilishwa katika vyombo vyahabari.Anaendelelea kusema kuwa utakuwa mpokeaji mwema,hadhira nzuri na mtumizi bora wa vyombo vyahabari ikiwa utaelewa zaidi kuhusu vyombo vyahabari. Uchanganuzi Hakiki Usemi ni mbinu ya mwingiliano wa uchanganuzi wa matini. Matini ni rekodi ya mawasiliano inayohusu uwasilishaji wa imani za kweli na ujenzi wa utambulisho wa wahusika (Taiwo, 2005).

Kwa hivyo Uchanganuzi Hakiki Usemi huchanganua usemi kutafuta maana fiche. Usemi hu ulichangia nadharia tete kuwa lugha haiwezi kujitokeza yenewe, hujitokeza kama kiwasilisho cha kipengele cha isimu kinachoonyesha ushindani wa uwezo katika jamii. Kutokana na kauli kuwa Uchanganuzi Hakiki Usemi huchanganua usemi ili kupata maana fiche, utafiti huu uliohusisha tasfida, tulitumia Uchanganuzi Hakiki Usemi kutoa maelezo kuhusu tasfida hizo zilizotumika katika kipindi cha *Connect* cha K24. Tasfida zilizotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha K24 ziliorodheshwa na kuelezwu kama jinsi mwasilishi alivyowasilisha kazi yake katika kipindi hiki cha *Connect*. Pia tulitumia nadharia hiyo ya Uchanganuzi Hakiki Usemi kuonyesha jinsi tasfida zilizotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24 zinavyosawiri jinsia.

Van Dijk anasema kuwa nadharia ya uchanganuzi huzingatia matatizo mbalimbali ya kijamii na hivyo huchanganua mtazamo wa wale ambao hutwezwa na kuchanganua jukumu la vipengelee mbalimbali vyahugha vinavyotumiwa katika kuhalalisha ngazi za kiutawala na kulinganisha na wanomimiliki maamlaka, njia na nafasi za kushuluhisha matatizo haya. Utafiti huu ulichunguza iwapo tasfida za kujamiihana zilizotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24 zinasawiri jinsia au la.

## **SURA YA TATU**

### **MBINU ZA UTAFITI**

#### **3.1. Utangulizi**

Sura hii inashughulikia jinsi utafiti wenyewe ulivyofanywa. Inaangazia mahali halisi ambapo data ya utafiti ilikusanywa, walengwa au kundi, uteuzi wa sampuli, muundo au aina ya utafiti, mbinu za kukusanya data zilizotumiwa na jinsi data ilivyochananuliwa.

#### **3.2 Mahali pa Utafiti**

Utafiti huu ulifanywa katika kipindi cha ‘*Connect*’ cha runinga ya K24. Mtafiti alilenga kukusanya tasfida za kujamiihana zilizotumiwa katika kipindi cha ‘*Connect*’ cha runinga ya K24. Ukusanyaji wa data ulifanywa kwa muda wa miezi tisa, kati ya mwaka wa 2011 na 2012.

#### **3.3 Kundu la Utafiti au Walengwa**

Utafiti huu ulilenga kutafiti tasfida za kujamiihana zilizotumiwa katika kipindi cha ‘*Connect*’ cha runinga ya K24. Pia ulilenga watazamaji wa kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24.

#### **3.4 Uteuzi wa Sampuli**

Uteuzi wa sampuli uliongozwa na madhumuni ya utafiti, kutambua na kueleza tasfida za kujamiihana zilizotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24 na kujadili swala la jinsia katika tasfida za kujamiihana zinazotumiwa katika kipindi cha ‘*Connect*’ cha runinga ya K24. Sampuli katika utafiti huu iliteuliwa kimakusudi. Mtafiti pia aliteuwa runinga ya K24 kimakusudi kwa sababu huwafikia watu wengi nchini na ndio iliyokuwa na data ya tasfida aliyoitaka na ingeweza kuafikia majibu ya maswali ya utafiti. Mtafiti alirekodi vipindi kumi kati ya mwaka wa elfu mbili na kumi na moja na elfu mbili na kumi na mbili.sampuli hii ya vipindi vitano ilimwezesha kuweka data katika muktadha wake.

### **Jedwali 1: Sampuli ya Vipindi vya Connect Vilivvoteuliwa**

KIPINDI CHA CONNECT	TAREHE	MADA	SAA
1	13/05/2011	<i>How to negotiate Mombasa raha contract</i>	10-11 usiku
2	21/05/2011	<i>Love tips part 1</i>	10.00-11.00 usiku
3	18/06/2011	<i>Hygiene (How to clear Miss Victoria)</i>	10.00-11.00 usiku
4	4/09/2011	<i>Mombasa raha positions</i>	10.00-11.00 usiku
5	24/01/2012	<i>Mombasa raha part 2</i>	10.00-11.00 usiku

Tulidhamiria kuchagua vipindi hivi vitano kati ya kumi tulivyoteua. Hii ni kwa sababu hivi ndivyo vilielekea kuwa na idadi kubwa ya data ya tafsida, tulizohitaji kuzitumia katika utafiti wetu.

### **3.5 Muundo wa Utafiti**

Utafiti huu ni wa kimaelezo na hii ni kwa sababu ulilenga kuhakiki tasfida za kujamiihana kama zilivytumiwa katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24.

### **3.6 Ukusanyaji wa Data**

Data katika utafiti huu ni tasfida za kujamiihana zinazotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24. Mtafiti alitazama, kunasa na kurekodi vipindi kumi vya *Connect* ili kupata na kunakili tasfida za kujamiihana zinazotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24. Mtafiti alinakili mazungumzo katika vipindi hivyo ili kudhihirisha matumizi ya tasfida hizo za kujamiihana katika muktadha. Kila kipindi kilikadiriwa kutumia saa moja. Mbinu ya mahojiano ilitumika. Mtafiti alimtembelea mwasilishaji wa kipindi Bi. Getrude Mungai na kumhoji. Mahojiano hayo yalirekodiwa katika kinasa sauti na kunakiliwa katika madaftari. Mtafiti alikuwa amenakili maswali ya kumwuliza mwasilishaji katika daftari lake. Mtafiti pia alifanya utafiti wake katika maktaba ili kupata yale yamefanywa kuhusu tasfida, jinsia na nadharia ya utafiti ya uchanganuzi hakiki usemi (UHU) na pia alitumia mbinu ya kudurusu mtandao na kutazama vipindi hivyo katika ‘youtube’.

### **3.7 Uchanganuzi wa Data**

Madhumuni ya utafiti yalikuwa kutambua na kueleza tasfida za kujamiihana zinazotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24 na kujadili swali la jinsia katika tasfida hizo za kujamiihana.

Katika kuchanganua data ya tasfida za kujamiihana katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24, tulizingatia hatua zifuatazo;

- i. Kutafsiri matini za tasfida kutoka lugha ya Kiingereza hadi lugha ya Kiswahili.  
Tafsiri hii ilikuwa muhimu kwa sababu nyingi yazo ilikuwa katika lugha ya Kiingereza na kazi hii iliandikwa katika lugha ya Kiswahili.
- ii. Kutambua kwa kupigia mstari tasfida za kujamiihana kutoka kwa matini iliyonakiliwa.
- iii. Kutambua na kufasiri tasfida za kujamiihana zilizotumiwa katika kipindi cha *Connect* na kuziweka katika majedwali.
- iv. Kuchanganua data ya tasfida za kujamiihana zilizofasiriwa ili kutathmini kama zilisawiri jinsia au la.

## **SURA YA NNE**

### **UCHANGANUZI WA DATA NA MATOKEO YA UTAFITI**

#### **4.1 Utangulizi**

Sura hii ya nne imegawanywa katika sehemu nne. Sehemu ya kwanza mmeorodheshwa na kutoa maelezo ya istilahi za tasfida ambazo ziliwekwa katika makundi matano. Sehemu ya pili inahusu mwasilishaji jinsi anavyothihirisha uwezo wake katika kuwasiliana na matumizi ya tasfida katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24 na muktadha wa matumizi ya tasfida hizo za kujamiihana. Sehemu ya tatu inahusu jinsi matumizi ya tasfida hizo inavyosawiri swala la jinsia.

#### **4.2 Tasfida**

Tasfida zilizotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha K24 tuliziweka katika makundi matano na kuzipa vichwa vidogo vidogo kulingana na sifa na uamilifu wake.

##### **4.2.1 Tasfida za Kuumeni.**

Katika utafiti wetu tuligundua tasfida tatu muhimu zilizoegemea uumeni.

###### **Jedwali la 1 istilahi za kurejelea uumeni.**

<b>Tasfida</b>	<b>Tafsiri</b>
<i>Mr Victor</i>	Dhakari.
<i>Safari Fupi</i>	Kumwaga manii kabla ya wakati ( <i>premature ejaculation</i> ).
<i>Pedicure</i>	Usafi wa miguu kwa kukata kucha na kuzipaka rangi. Kusafisha sehemu za mwili wa mwanamume zinazotumiwa wakati wa kujamiihana.

**Jedwali hili linaonyesha tasfida za kujamiihana zinazorejelea mwanamume ambazo ni tatu pekee.**

#### **4.2.2 Tasfida za Uukeni.**

Kuhusu tasfida za mwanamke tuligundua zilikuwa nyingi na ni kama zifuatazo.

#### **Jedwali la 2 Istilahi za kurejelea uukeni.**

<b>Tasfida</b>	<b>Tafsiri</b>
<i>Miss Victoria</i>	Uke
<i>Dashboard</i>	Matiti
<i>Pleasure knob</i>	Kinembe/ kisimi
<i>Supporting documents</i>	Makalio na kiuno/ kiweo
<i>Juicy spots</i>	Sehemu za mwili zinazoguzwa na kusababisha msisimko wa kimahaba
<i>Charcoal burner</i>	Kifaa kinachotumiwa kunukiza au kubadilisha harufu inayotoka <i>Miss Victoria</i>
<i>Smoking the house</i>	Kunukiza/ kufanya chumba kiwe na harufu nzuri ili kumvutia mwanamume.
<i>Vanilla</i>	Lavani/ kiungo kinachotumiwa kunukiza <i>Miss Victoria</i> .
<i>Mercedes Benz</i>	Mwili wa mwanamke
<i>Athi River</i>	Mapajani.
<i>Miss Victoria PH</i>	Kiwango cha joto ya uke ( <i>Miss Victoria</i> ).
<i>Ponytail</i>	Nywele za sehemu za siri za mwanamke .

Jedwali hili linaonyesha tasfida za kujamiihana zinazorejelea au kuegemea ukeni na ni nyingi zikilinganishwa na zile za kurejelea uumeni.

Tasfida za kujamiihana zinazorejelea mwanamke ni kumi na mbili ilhali zile zinazorejelea mwanaume ni tatu.

#### 4.2.3 Tasfida za Mitindo au Jinsi ya Kujamiiana

Tuligundua kuwa mwasilishi alitumia istilahi nyingi kueleza mitindo au jinsi/njia za kujamiiana.

##### Jedwali la 3

###### Tasfida za mitindo au jinsi ya kujamiiana

Tafsida	Tafsiri
Kuchuna mboga	Kujamiiana kama mbwa (dog style).
<i>Nyambura style</i>	Mwanamume juu na mwanamke chini, mtindo wa kawaida, unaochosha (missionary style).
Woyee	Mtindo wa kuinua miguu miwili Wanapojamiiana.
<i>Rabbit style.</i>	Mtindo kama ule wa mbwa lakini hakuna kutingisika. (unachosha).
A river au kuogelea	Punyeto (masturbation).
<i>360 position</i>	kule kuzunguka huku mnafanya mapenzi.
Set of four	Kuchezea kichwa cha dhakari, kupenyeza kidogo kwenye uke, kuingiza ndani ya <i>Miss Victoria</i> kwa mara nne nne.
<i>T Style</i>	Kule kujamiiana ukiwa katika upande (across).
<i>Mode of Transport.</i>	Jinsi ya kufanya mapenzi au jinsi ya kusafiri katika kujamiiana .
<i>Fly to Mombasa raha.</i>	Njia ya haraka ya kujamiiana au kufanya

	Mapenzi haraka bila kujitayarisha vivilivo
<i>Taking a train to Mombasa raha.</i>	Njia ya polepole ya kujamiihana.
<i>Taking a personal car.</i>	Njia nzuri ya usafiri ambayo unaweza kupumzika popote utakapo.
<i>Plough</i>	Kuwekeleana miguu. Kuweka mguu juu ya mwingine.
<i>Foreplay</i>	Kucheza au kugusa sehemu mbalimbali za Mwili ili kutayarisha kujamiihana.
<i>Kamata bonnet</i>	Kujamiihana kwa haraka mwanamke akiwa ameshika boneti.

Jedwali hili linaonyesha tasfida za mitindo na jinsi ya kujitarishia kujamiihana. Tasfida hizi ni kumi na sita na katika maelezo yake baadaye zatarajiwa kudhihirisha masuala muhimu kuhusu mwanamme na mwanamke.

#### **4.2.4 Tasfida za Tendo la Kujamiiana.**

Tuligundua tasfida tatu zilitumiwa kurejelea tendo la kujamiiana.

#### **Jedwali la 4**

##### **Tasfida za tendo la kujamiiana.**

<b>Tafsida</b>	<b>Tafsiri</b>
<i>Mombasa raha</i>	Nongo au kujamiiana ( <i>sex</i> ).
<i>Mombasa raha trip</i>	Kujamiiana kwenyewe ( <i>sexual intercourse</i> ).
<i>Mombasa raha first class</i>	Nongo nzuri kabisa.

Jedwali hili linaonyesha tasfida za kitendo chenyewe cha kujamiiana. Tasfida hizo zilikuwa tatu tu ambazo ni *Mombasa raha*, *Mombasa raha trip* na *Mombasa raha first class*.

#### **4.2.5 Tasfida Nyinginezo**

Tuligundua kuwa kulikuwa na tasfida ambayo tusingeiorodhesha kwenye makundi manne tuliyoyataja hapo awali na tukaiweka kwenye kikundi cha istilahi nyinginezo.

#### **Jedwali la 5**

##### **Tasfida nyinginezo**

<b>Tafsida</b>	<b>Tafsiri</b>
<i>Foot and mouth</i>	Ugonjwa unaoweza kutokea kutokana na uchafu, hasa kwa sehemu za mwili za mwanamke, kama vile vidole vyatya miguu vyatya mwanamume vinavyotumiwa kisugulia kinembe.

Jedwali hili linaonyesha tasfida moja ya kujamiihana ambayo isingeorodhesha katika makundi yaliyotangulia.

Tasfida hizi tulizitambua, tukazijadili na kuzichanganua kwa undani moja baada ya nyingine tukiegemea vichwa mbalimbali, ufaafu wazo katika vichwa hivyo na kuziweka katika miktadha wa matumizi yazo.

#### **4.3 Mwasilishaji na Muktadha wa Matumizi ya Tasfida.**

Katika sehemu hii tulitathmini mwasilishaji na muktadha wa matumizi ya tasfida tukiongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi (UHU), nadharia ambayo mihimili yake mikuu ni Uhakiki, Itikadi na Uwezo. Nadharia hii inadokeza kuwa usemi hufungamana na muktadha wa kihistoria. Hii inamaanisha kuwa ili usemi ueleweke lazima uhusishwe na muktadha wa kitamaduni. Mwasilishaji lazima aonyeshe uelewa wa itikadi za kijamii ili aweze kuwasilisha kazi ambayo inawiana na muktadha wa kijamii.

Uhakiki ni kule kuangalia usemi au matini kwa jicho la upekuzi kuweka wazi hali zote pasi kuegemea upande wowote. Istilahi za tasfida zilizotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24 na mwasilishaji zilichambuliwa bila kuegemea upande wowote na kuziorodhesha jinsi zinavyojitokeza. Katika uteuzi wa istilahi za tasfida mwasilishaji amezingatia itikadi inayomaanisha mawazo pendwa yanayoendelezwa na jamii. Itikadi za Kiafrika ni zile ambazo zimemweka mwanamume mbele ya mwanamke. Jambo ambalo limemfanya mwanamume kumdhibiti mwanamke na limehalalishwa.

Uwezo ni swala lingine muhimu ambalo linazingatiwa katika nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi. Nadharia hii huchunguza jinsi jinsia inavyoendelezwa na kuonyesha ni jinsia gani yenye mamlaka na ushawishi kuliko nyingine. Uchanganuzi Hakiki Usemi huchanganua lugha ya wenye mamlaka na wanavyowajibika kwa kutokuwepo na usawa na wale walio na namna na nafasi za kuboresha hali hizo. Mwasilishaji wa kipindi cha *Connect* cha Runinga ya K24 nchini Kenya ni mwanamke. Kipindi hiki huwasilishwa na watu wawili ambao wote ni wanawake.

Mwasilishi wa pili kazi yake ni kuingiliana na mwasilishi mkuu. Yeye pia huchukua nafasi ya hadhira na katika kujadiliana uhusika huu unarahisisha mawasiliano. Mwasilishaji alidhihirisha uwezo wake alipoyazungumzia maswala ya kujamiihana bila woga wowote. Aliyazungumzia maswala ya kujamiihana kama swala lingine lolote katika jamii bila kufedheheka.

Uwezo huu wake unakiuka kaida za kitamaduni ambazo haziwaruhusu watu kuzungumzia maswala ya kujamiihana hadharani. Katika jamii za kiafrika mwanamke hafai kuzungumza mbele ya mwanamume ilhali mwasilishaji amevuka mipaka hata kuyajadili mambo ya kujamiihana katika runinga ya K24.

Tuliangazia kuwa ujasiri aliokuwa nao mwasilishaji ambao si wa kawaida katika jamii ya Kiafrika hasa ikilinganishwa kuwa yeye ni mwanamke. Wanawake wengi wa Kiafrika ni waoga na hawawezi kuzungumzia maswala ya kujamiihana hadharani. Mwasilishi ni dhihirisho tosha la uwezo alionao mwanamke wa Kiafrika ingawa amedhalilishwa na kuonekana kana kwamba yeye ni bure. Tulijaribu kubaini uwezo wake aliouonyesha katika ufasaha wake kutumia, lugha mbili Kiingereza na Kiswahili, ule ucheshi na matumizi ya ishara alipokuwa akielezea maswala nyeti na sehemu muhimu za mwili. Na uwezo wake katika uteuzi wa tasfida alizozitumia. Aliteua tasfida za kipekee ambazo kwa hakika ukiziweka kwenye uzani utatambua uwezo usio wa kawaida hasa kwa mwanamke ambaye amechukuliwa kuwa duni na mdhaifu katika jamii ya Kiafrika, uteuzi wake wa tafsida ulitegema uelewa wake wa mazingira na muktadha wa nchi, kwa mfano, katika matumizi ya *Mombasa raha*, *Mombasa raha trip*, *Mombasa raha first class*, ukambani, Athi River. *Dashboard*, *Nyambura style*, kuchuna mboga, personal car na kadhalika.

**Kiamb. 1:** *Mombasa raha being a place of happiness all want to go to Mombasa raha, isn't it? But the approach and Mode of Transport is different (Mombasa raha kuwa ni mahali pa furaha, watu wote wangependa kuenda Mombasa raha au siyo, lakini mtazamo na jinsi ya kusafiri ni tofauti.)*

Mombasa ni sehemu ya nchi ya Kenya ambayo huwa upande wa pwani. Ni sehemu ambayo imezungukwa na Bahari ya Hindi. Hii ni sehemu ambayo hujulikana kwa raha na watu wengi huenda Mombasa kujivinjari wakati wa likizo. Watu wengi huenda kule kuogelea, kula vyakula vya kifahari na pia kupunga upopo ule wa bahari. Huwa kuna feri ambazo huvusha watu kutoka upande mmoja wa bahari hadi mwingine. Watu wengi huchukua familia na wapenzi wao kwa muda wa siku kadha au majuma kwa mapumziko kwa hivyo Mombasa hujulikana sana kwa ajili ya raha. Watu wengi huweka akiba ya kutosha ili wapate hela za matumizi wanapoenda Mombasa.

Mwasilishaji alipotumia *Mombasa raha* kuelezea kujamiihana ni dhihirisho tosha kuwa alielewa jinsi Wakenya huchukulia Mombasa kuwa muhimu na ni sehemu ya raha. Hivyo basi alilinganisha raha inayopatikana Mombasa na tendo la kujamiihana na ikawa ni kivutio kikubwa. Ule uwezo wake wa kulinganisha kujamiihana na *Mombasa raha* ni wa kipekee na kuonyesha kuwa mwasilishaji si mwanamke wa kawaida. Yeye ni mwanamke aliye na ufahamu wa hali ya juu wa mazingira, na miktadha inayopendwa na watu wengi.

*Mode of Transport* ni njia au jinsi ya kusafiri. Kuna njia nyingi za usafiri ambazo zinaweza kuwa za haraka, kadri au polepole. Uamuzi wa kuteua njia ya usafiri humtegemea msafiri, kama ana haraka anaweza kutumia ndege, kama hana haraka sana anaweza kutumia basi au gari la kibinafsi na kama hana mbio anaweza kutumia gari la moshi. Kwa hivyo usafiri wa kwenda Mombasa, safari ambayo ni nefuhumtegemea msafiri kama ana haraka au hana haraka.

Mwasilishaji alipotumia istilahi *Mode of Transport* alimaanisha jinsi ya kufanya mapenzi au njia ya kufanya mapenzi. Alieleza kuwa njia ya haraka ya kujamiihana haiwezi kutoa matokea mwafaka. Alieleza kuwa njia ya polepole pia haingeweza kufanikishakujamiihana. Tuligundua kuwa alihimiza njia ya kadri ambayo ni matumizi ya gari la kibinafsi. Matumizi ya gari la kibinafsi huwa ni sambamba kwa sababu msafiri atatumia apendavyo, hivi kwamba akitaka kupumzika popote njiani atakuwa na uhuru wa kufanya hivyo.

Mwasilishaji alielewa vizuri muktadha na mazingira ya watazamaji wake na ndiposa aliweza kuteua istilahi ya *Mode of Transport* kwa sababu alijua kuwa watazamaji wake wangemwelewa bila matatizo yoyote. Alifahamu vyema kuwa akieleza njia ya kupaa watazamaji wangelewa ni njia ya haraka sana ya usafiri (kujamiihana). Matumizi ya gari moshi alifahamu kuwa watazamaji wangelewa ni njia ya polepole sana na ambayo huchosha sana kwa wasafiri. Uteuzi wake wa gari la kibinafsi alijua ni njia mwafaka ya usafiri na akawa akiwahimiza wanandoa kutumia njia hiyo ya gari la kibinafsi kusafiri Mombasa. Tuligundua kuwa alitaka kuwafunza watu njia ya kadri ya usafiri ndiyo iliyofaa katika kujamiihana.

**Kiamb. 2:** *I smoke myself, my room and actually my husband associates this smell with Mombasa raha trip, you know he comes, I do abit of udi nakwambia za Kikikuyu zinasimama.* (Ninajifukisha, nafukisha chumba change na kwa hakika mume wangu huhusisha harufu hii na safari ya *Mombasa raha*, unajua anapokuja na nimefukisha udi hupandwa na jazba za Kikuyu)

Safari ya kwenda Mombasa kwa mtu aliyetoka Bara si karibu. Inajulikana kuwa Mombasa ni kilomita mia tano kutoka Nairobi, kwa hivyo si safari fupi. Watu wanapoipanga kwenda Mombasa hubidi wafanye matayarisho kabambe. Lazima wajitayarische kwa hali na mali

kama wangetaka kufika Mombasa. Fedha huhitajika kwa wingi na pia hali sawa ya kiafya ni lazima.

Ni muhimu pia mtu ajue jinsi atakavyosafiri, afanye uamuzi kama atatumia gari la kibinafsi, basi, ndege au gari la moshi, uamuzi wa m safiri ni muhimu sana kama angetaka kufika Mombasa kwa hivyo kwenda Mombasa si jambo la kufanyiwa mzaha ni sharti matayarisho mwafaka yafanywe.

Tuligundua katika utafiti wetu kuwa kwa mwasilishaji kulinganisha safari ya Mombasa na matayarisho katika kujamiihana ni dhihirisho kuwa kujamiihana si swala la kufanya mzaha. Wahusika hawana budi kujitayarisha vilivyo ili safari yao iweze kufanikiwa. Alieleza kuwa ili kufika *Mombasa raha* ni lazima safari ipangwe vilivyo. Wahusika wasipojitayarisha vilivyo hawatafikia raha iliyokusudiwa katika kujamiihana.

**Kiamb. 3:** *I am buying you a car Mombasa raha first class, no, kamata bonnet, bonnet can only be a car.(Ninakununulia gari *Mombasa raha* first class, la, shika bonneti, boneti inaweza tu kuwa gari)*

*Mombasa raha* First Class inamaanisha kufikia matarajio na matamanio ya kujamiihana. Ni kule kufaulu kwa safari na kupata matokeo mazuri kama ilivyotarajiwa. Mwasilishaji alieleza kuwa ili *Mombasa raha* iwe `first class` lazima matayarisho yafanywe vilivyo na uamuzi wa usafiri uwe ni ule wa gari la kibinafsi ( personal car). Ule uwezo wa kuita kujamiihana kuzuri kabisa kuwa *Mombasa raha* first class ni dhihirisho la uteuzi mwafaka wa istilahi kwa ustadi usio wa kufananishwa na wa mtu mwengine.

**Kiamb. 4:** *Men would prefer, you understand, to fly to Mombasa raha and when they fly they miss out so many things on the way. (wanaume wangependa unaelewa, kupaa kwenda *Mombasa raha* na wanapopaa wanakosa vitu vingi njiani)*

Flying to *Mombasa raha* ni njia ya haraka ya kwenda Mombasa. Kwa kupaa au kutumia ndege, msafiri huchukua muda wa dakika arobaini na tano kufika Mombasa. Hii ndiyo njia ya haraka zaidi ya kufika Mombasa. Watu wengi amba wana vyao (matajiri) husafiri kwa ndege kwenda Mombasa kwa sababu ni rahisi na haiwachoshi.

Mwasilishaji alipotumia istilahi Fly to *Mombasa raha* alimaanisha kuwa ni njia ya haraka sana ya kujamiihana. Alieleza kuwa ni njia ambayo msafiri huenda Mombasa moja kwa moja

bila kusita wala kusimama njiani. Tuligundua kuwa alimaanisha kujamiiiana kwa haraka ambako kuna uwezekano wa mwanamume kumwaga manii kwa haraka ilhali akimwacha mwanamke akinining`inia. Hii ni kwa sababu, mwili wa mwanamke haukufanyiwa matayarisho kambambe ya kukabiliana na kujamiiiana. Uelewa wa mwasilishaji wa muktadha na mazingira ulimsaidia kuteua istilahi *Fly to Mombasa raha* kama njia ya haraka ya kufanya mapenzi na ambayo haifiki matamanio ya wahusika. Hii ni kwa sababu, usafiri kuwa wa haraka na hutakuwa kufurahia kwa mazingira na kuifahamu miji mbalimbali iliyo njiani kama vile Ukambani na Athi River. Hii ni kwa sababu msafiri atapitia angani na hataweza kutua sehemu mbalimbali kuzifurahia. Ingawa msafiri atakuwa amefika *Mombasa raha*, hatakuwa amefurahia mazingira ya njiani. Tuligundua kuwa ingawa *Fly to Mombasa raha* ni njia ya haraka ya kujamiiiana haifiki madhumuni ya kujamiiiana vilivyo kwa sababu tendo lenyewe ni la haraka sana.

**Kiamb. 5:** *Women on the other hand, would like to take a train, I mean how many hours, 12 hours and do you know how many stops on the way, I think over 10.(Wanawake kwa upande ule mwingine wangependa kwenda *Mombasa raha* lakini wangependa kutumia gari la moshi, namaanisha masaa mangapi, kumi na mawili na unajua wanasimama mara ngapi njianai, nafikiria zaidi ya kumi)*

Taking a Train to *Mombasa raha* ni njia ya usafiri ya kutumia gari la moshi kwenda Mombasa ni njia ya polepole sana, ambayo huchukua muda wasiku mbili kutoka Nairobi. Njia hii ni ya polepole sana na ni rahisi kutibuka kabla ya kufika Mombasa. Mwasilishaji alelewa kuwa kutumia gari la moshi ni njia ya polepole sana na ambayo inachosha sana na hata msafiri anaweza kupoteza matumaini ya kufika Mombasa mji wa raha njiani. Kwa kuelewa mwendo wa gari la moshi mwasilishaji aliweza kulinganisha usafiri huo wa polepole na kujamiiiana kwa polepole sanaambako wahusika huchukua muda mrefu njiani au katika matayarisho na huwa kuna uwezekano wa kujamiiiana kule kutibuka kabla ya kuafikia madhumuni yake.

Uteuzi wa istilahi Taking a train to *Mombasa raha* kama njia ya polepole ya kujamiiiana ni dhihirisho la uelewa wake wa mazingira, kuwa kwenda *Mombasa raha* kwa gari la moshi kunawachukuwa muda mrefu na kunachosha sana. Uelewa wake wa mazingira na muktadha ulimwezesha kuwatahadharisha wahusika wa kujamiiiana kutotumia njia hiyo ya gari la

moshi kusafiri, kwa sababu kuna uwezekano wa safari yenewe kutibuka au kutoafikia madhumuni yake.

**Kiamb. 6:** *You can compromise and take a personal car, there is so much you can do, you can determine the speed on the way, you can have stops on the way. Do you want to stop around ukambani area where you can buy bananas, oranges, pawpaws, hohos or want to go straight down. (Mnaweza kukubaliana na kuchukua gari la kibinagsi, kuna mengi mnaweza kufanya, unaweza kuamua kasi au mahala pa kusimama kule ukambani ambapo utaweza kununua ndizi, machungwa, paipai, pilipili hoho au unataka kwenda moja kwa moja chini).*

Personal car ni gari la kibinagsi ambalo mwenyewe anaweza kulitumia apendavyo. Mwasilishi alipotumia personal car kama njia moja ya kusafiri kuenda *Mombasa raha*, alionyesha kuwa ni njia mwafaka kwa sababu mtumizi ana uhuru wa kulidhibiti gari apendavyo. Hivi kwamba akitaka kusimama njiani atafanya hivyo bila vikwazo vyovyyote. Pia akitaka kwenda kwa kasi au polepole atakuwa ni uamuzi wake.

Mwasilishi alielewa vyema kuwa watu wengi wanapotaka kwenda Mombasa kujiburudisha wengi wao hutumia magari ya kibinagsi au hata kukodisha gari la kusafiria ili waweze kusafiri kwa starehe zao. Alionyesha uelewa mwema wa mazingira na muktadha na ndiposa anatumia istilahi personal car kuelezea njia ya kusafiri *Mombasa raha*. Alielewa kuwa watu wengi hujisikia wametosheka wanapolitumia gari la kibinasfi wanaposafiri kwenda safari ya mbali, ambapo watakuwa na uhuru wa kusafiri na kuenda popote watakapo kwa sababu kwa kutumia personal car personal car hatachelewa anapoenda kama gari lake liko katika hali nzuri. Ule uelewa wa mwasilishi wa muktadha unamwezesha kueleza jinsi watu wanavyoweza kujamiiiana kwa njia inayofaa kwa mwendo wao wenyenewe kama vile gari la kibinagsi hutumika na wenyewe wapendavyo. Kumaanisha ukasi na upole wa kujamiiiana utaweza kudhibitiwa na dereva (mwanamume)

Katika safari ya kwenda Mombasa kuna miji mingi ambayo watu hupitia. Sehemu mojawapo muhimu ni Ukambani, kwa sababu huwa ni safari ndefu hubidi watu wapumzike kwa mfano katika Motito wa Ndei au Emali kupata kikombe cha chai au chakula ili kuongeza nguvu za kuendelea na safari.

Mwasilishaji alidhihirisha uwezo wake wa uteuzi wa istilahi kwa kutumia vituo hivyo vya Ukambani kuonyesha sehemu za mwili wa mwanamke ambazo mwanaume anaweza kutulia na kuzigusagusa ili kuleta mchemko wa kimahaba kwa mwanamke. Alilinganisha Ukambani na sehemu ya matiti ya mwanamke. Hii ni sehemu muhimu ambayo mwanamume anaweza kutulia na kuchezacheza nayo anapoelekea kujamiiana na mwanamke.

**Kiamb. 7:** *Today we decide to take a personal car to Mombasa raha we are taking a Mercedes Benz. For you to use a Mercedes Benz to go to Mombasa raha you do not just jump into the car and drive off and if you do hautafika mahali nakwambia utaishi njiani labda hata athi river, you may be lucky if you fika athiriver maybe mlolongo. (Leo tumeamua kuchukua gari la kibinafsi kuenda Mombasa raha, na tunachukua Mercedes Benz. Ili utumie Mercedes Benz kenda Mombasa raha hauwezi kuingia gari tu na kuondoka, ukifanya hivyo hautafika mahali, utaishia njiani labda athi river kama utabahatika labda utafika tu mlolongo.)*

Athi-River ni sehemu ambayo haiko mbali sana na Nairobi. Mwasilishaji alieleza kuwa hii pia ni sehemu ambayo wasafiri wanaweza kupumzika kidogo katika safari yao ya kwenda Mombasa raha. Alieleza kuwa Athi River ni sehemu ya mapaja ya mwanamke .Alieleza mwanamume hana budi kuchukua muda wake kugusagusa mapaja ya mwanamke anapoelekea katika safari ya kujamiiana.

Uelewa wa mwasilishaji wa itikadi za Wakenya zilimsaidia sana katika kuwasiliana kuhusu kujamiiana, kuelewa kuwa watu wanapenda sana kwenda Mombasa kujivinjari kulimsaidia kuweza kuteua istilahi ambazo zinaafiki mila na desturi za Kiafrika. Imani kuwa Mombasa ni mji wa raha imeshikiliwa na wengi sana hivi kwamba hata watalii kutoka nchi za nje wamefika nchini, wengi hutembelea Mombasa kama sehemu moja ya kujivinjari na kuogelea kwenye bahari. Kutokana na uelewa huu na uteuzi wake mwafaka wa istilahi, kipindi hiki chake cha *Connect* cha runinga ya K24 kilishabikiwa na wengi nchini Kenya na pia nchi za nje. Uteuzi wake wa Istilahi za tasfida pia uliegemea vitu ambavyo watu huvionea fahari na kazi wanazozifanya na aliweza kuzitumia istilahi hizo vizuri ajabu.

*Mercedes Benz* ni aina ya gari la kifahari na lenye nguvu sana. Mtu anapobebwa kwagari hili hujiskia ametosheka, hachoki wala hatamani kushuka. Gari lenyewe hupanda mlima kama ni mteremko. Gari hili huendeshwa na watu matajiri kwa kuwa ni ghali na hugharimu

zaidi ya shilingi milioni moja. Aina hii ya gari ndilo humbeba rais na viongozi mashuhuri nchini Kenya. Kwa mwasilishaji kuuita au kuupa mwili wa mwanamke jina *Mercedes Benz* alionyesha kuelewa mazingira ya watazamaji wake ambao walielewa *Mercedes Benz* ni gari la aina gani. Tuligundua kuwa alitaka kuonyesha thamani ya mwili wa mwanamke, kuwa mwanamke ni muhimu sana na sio wakuchezewa ovyoovyo. Uteuzi wake na tasfiri hiyo *Mercedes Benz* kurejelea mwili wa mwanamke alionyesha uelewa wake wa jinsi watu huchukulia aina hii ya gari.

**Kiamb.8:** *When you are checking the dashboard, just make sure everything is okay.* (Wakati unaangalia ‘*dashboard*’ hakikisha kila kitu kiko sawa.)

*Dashboard* ni sehemu ya mbele ya gari ambayo huwa ni muhimu sana kuwezesha gari kuendeshwa. Alilinganisha sehemu ya mbele ya gari na matiti. Tuligundua kuwa alichukulia matiti kama injini ya mwili wa mwanamke ambayo inapoguswa huibua hisia kali zinazochochea mahaba. Hii ina maana kuwa mwanamume anapogusa matiti ya mwanamke ni kana kwamba anauwasha moto mwili wa mwanamke ikilinganishwa na kuwa injini inapowashwa gari lazima lingurume na kuanza mwendo. Watu wengi huifahamu sehemu ya mbele ya gari (*dashboard*) na hujua kuwa hitilafu yoyote ikitokea kwa gari lazima boneti ifunguliwe ili uchunguzi ufanywe na hitilafu hiyo kushughulikiwa na kurekebishiwa. Kwa hivyo matiti ni muhimu sana na ni lazima yaguzwe ili yachoochee hisia ambayo itamfanya mwanamke atamani kujamiiiana. Mwasilishi alieleza kuwa si vizuri kuanza kujamiiiana moja kwa moja, inabidi hisia ziibuliwe za kimahaba kwanza ili kujamiiiana kufurahiwe na pande zote mbili.

**Kiamb. 9:** *Many women like Nyambura, the missionary style ingawa there are other styles like kuchuna mboga, oiyee, rabbit.* (Wanawake wengi wanapenda nyambura, mtindo wa kimishonari ingawa kuna mitindo minginekama vile kuchuna mboga, oiye, rabbit.)

*Nyambura style* ni jina la kawaida la mwanamke nchini Kenya. Huhitaji kuelezea Nyambura ni nani katika jamii ya Kiafrika hasa nchini Kenya. Nyambura hutumika kumrejelea mwanamke awe yejote yule. Kwa sababu hili ni jina la kawaida la kumrejelea mwanamke na linajulikana kote, kwa mwasilishi kuteua jina hili *Nyambura style* kuonyesha mtindo wa kawaida au wa zamani kufanya mapenzi.

Alielewa fika kuwa kulingana na Wakenya isingekuwa vigumu kuelewa mtindo huu. Hii ni kwa sababu watu wengi wanajua jina Nyambura pia alielewa kuwa jina Nyambura linapendwa na watu wengi nchini Kenya na kwa kulitumia, alitaka kuonyesha kuwa mtindo huu hupendwa na watu wengi na ndio hutumiwa sana na wanajamii katika kujamiihana, ni kutokana na uzoefu wa matumizi ya mtindo huu ambapo mwasilishi aliingilia kati kuzua mitindo mingine ambayo inaweza kutumiwa katika kujamiihana ili wanandoa wafurahie kitendo hiki cha ndoa. Mitindo mipya aliyoizua na kuwafunza wanandoa katika runinga ya K24 ni kuchuna mboga, 360 position, set of four, T style. Woyee, rabbit style na mingineyo.

Kuchuna mboga ni shughuli muhimu ambayo hufanywa na wanawake. Hii ni shughuli inayoelewka na watu wengi katika jamii ya kiafrika. Kwa hivyo mwasilishaji alipoteua kuchuna mboga kama istilahi mojawapo ya mitindo ya kujamiihana alielewa kuwa mtindo huo ungeelewka kwa urahisi. Hii ni kwa sababu mwanamke anapochuna mboga ni lazima ainame ili aweze kufikia zile mboga anazozichuna. Ni dhahiri kuwa katika mtindo huu wa kuchuna mboga mwanamume huingiza dhakari yake kwa sehemu ya siri ya mwanamke, mwanamke akiwa ameinama jinsi afanyakyo anapokuwa akichuna mboga. Kwa kutumia istilahi hii alionyesha uelewa wa mazingira kuwa isingewachukua wanajamii muda wa ziada kueleza ili kuelewa mtindo huo wa kuchuna mboga.

**Kiamb. 10:** *There are so many types of burners; an electric burner and a coal burner.*

*This is a charcoal burner. Chetezo ndogo cha makaa. (Kuna aina nyingi ya chetezo; kuna chetezo cha umeme na chetezo cha makaa. Hiki ni chetezo cha makaa, chetezo kidogo cha makaa.)*

Chetezo ni joto la uke (miss victoria). Chetezo hiki cha makaa na kufukisha nyumba ni kule kufukisha ule uke wa mwanamke kutoa harufu mbaya na kufanya uwe joto. Chetezo ambacho hutumia makaa hutumiwa na watu wengi wa Kenya katika upishi wao. Chetezo huhifadhi joto kwa muda mrefu. Kwa hivyo mwasilishi alipoteua istilahi *charcoal burner* alionyesha uelewa wake wa mazingira na muktadha. Tuligundua kuwa katika kutumia istilahi *charcoal burner* alielewa wakenya wanaelewa vizuri chetezo na matumizi yake. Tuligundua kuwa alielewa kuwa chetezo likiwashwa hutoa moshi ambaa husambaa kila mahali. Alitumia kifaa hiki kinachofahamika na kuonyesha jinsi mwanamke anavyoweza kukitumia kunukiza *Miss Victoria* ili iweze kumvutia mwanamume na kuondoa harufu mbaya. Uwezo wake ulithihirika kwa vile alionyesha kwa runinga jinsi ya kuwashaa

chetezo hilo kwa kutumia *Vanilla* na kuchuchumaa ili moshi uweze kupenyeza kunukiza *Miss Victoria*. Alithibitisha hayo kwa matendo na maneno aliyokuwa akiyazungumzia.

**Kiamb. 11:** *Turn to reverse cow girl and of course he will love this because really the supporting documents look good.* (Angalia nyuma na atapenda kwa kuwa the supporting documents zinakaa nzuri.)

*Supporting documents* ni sehemu ambazo ni muhimu na zinazochangia kufaulu kwa kujamiihana kama vile makalio na kiuno. Hizi ni sehemu ambazo mwanamume anapozinguzanguzahusaidia katika kuibua hisia za kimahaba na kumfanya mwanamke ahisi kujamiihana. Sehemu hizi ni muhimu kwa sababu ni visaidizi muhimu vya *Miss Victoria* ambavyo ni viungo muhimu sana katika kujamiihana.

Katika uhalisia wa mambo *supporting documents* huwa ni muhimu sana kwa mtu anapokuwa akitafuta kazi au kupandishwa cheo. Hivi ni vyeti vya ziada na barua ambazo mtu anayatafuta kazihuandikiwa na watu wenyewe vyeo kuonyesha utendazi kazi wake katika nyanja mbalimbali. Vyeti hivyo vinaweza kuwa vya uhusika wake katika michezo, kutoa msaada fulani na pia katika vikundi mbalimbali.

Vyeti hivyo na barua husaidia sana na wakati mwingine hutumika katika uamuzi wa wanaopata kazi au kupandishwa cheo. Mwasilishaji alipotumia *supporting documents* kueleza sehemu kama makalio na kiuno na kuzieleza kama muhimu sana katika kujamiihana alionyesha uelewa wake wa muktadha na mazingira ya Kenya hasa kikazi. Alielewa fika kuwa ili mtu kufaulu kupata kazi au cheo inabidi awe na nyongeza ya vyeti au barua za kuonyesha utendakazi wake. Tuligundua kuwa katika uteuzi wake wa istilahi *Supporting documents* alifahamu kuwa watazamaji wa kipindi chake cha *Connect* cha runinga ya K24 wangelewa kwa urahisi maana ya istilahi hiyo *Supporting documents* katika shughuli zao za kazini.

**Kiamb. 12:** *You oftenly hear a couple say oh he doesn't give me foreplay or she doesn't like foreplay.* (Mara nyingi utasikia wanandoa wakisema oh mume wangu hanipi ‘a foreplay’ au mke wangu hapendi ‘foreplay’.)

*Foreplay* ni kitendo cha kushikashika na kuchezacheza na sehemu za siri au viungo vinavyohusika na kujamiihana kama vile *Mr Victor, Miss Victoria, Dashboard, Supporting documents, Pleasure knob* na nyinginezo kabla ya kujamiihana. Mwasilishaji katika uteuzi

wake wa istilahi hii ya mchezo wa kutanguliza alionyesha uelewa wake wa muktadha wa kujamiiiana kuwa ni muhimu kujitayarishia kujamiiiana kwa kuchezeanachezeana kabla ya kitendo chenyewe cha kujamiiiana. Tuligundua kuwa alielewa kuwa wahusika wakienda moja kwa moja katika kujamiiiana bila matayarisho hawatafaulu katika kujamiiiana kwao. Kwa uelewa wake wa muktadha aliweza kusisitiza kuchezacheza na viungo vinavyohusika na kujamiiiana kabla ya tendo lenyewe ni muhimu sana.

**Kiamb. 13:** *Assuming that this is my husband and am going to borrow his toe, but by the time you put this toe in there , you better been have a pedicure otherwise you give foot and mouth disease, you ndont need this to happen.*

(Nikichukulia kuwa huyu ni mume wangu na ninaazima kidole chake, lakini kabla hujatia hicho kidole ndani pale, ni afadhali uwe umeshafanya *pedicure*, la sivyo utampa *Miss Victoria* ugonjwa wa miguu na mdomo ilhali hutaki hili kutendeka.)

*Pedicure* ni kushughulikia na kutibu miguu na kucha za miguu. Ni kule kusafisha miguu na vidole vyamwanamume kwa kukata kucha na kuzipaka rangi. Hili ni jambo ambalo hufanywa na watu wengi wanawake kwa wanaume ili kuhakikisha kuwa wako wasafi. Mwasilishaji alielewa vizuri kuwa akitumia istilahi *pedicure* angeeleweka vema. Hii ni kwa sababu usafi hufanywa na watu tofautitofauti katika vyumba vya urembo au saluni. Kwa kuwa *pedicure* hujumuisha kuondoa uchafu kwenye kucha, alielewa kuwa akiwaelezea watazamaji kuhusu usafi wa kucha zawa naume ili wasiambukize wake wao ugonjwa wanaposugua kinembe (*pleasure knob*) kwa vidole hivyo wakati wa matayarisho ya kujamiiiana angeeleweka vema. Tuligundua mwasilishaji alifahamu kuwa wanawake wengi ndio hushughulikia usafi huo na kwa kutoa mafunzo kuwa wanaume pia washughulikie usafi huo lilikuwa swala la busara na kuonyesha uelewa wake wa mazingira na muktadha.

*Foot and mouth* ni ugonjwa unaoweza kutokea kutokana na uchafu. Mwasilishaji alielewa kuwa ugonjwa huu wa *Foot and mouth* unaweza kuambukizwa mwanamke katika sehemu yake ya siri wakati mwanamume anatumia vidole vyake vya miguu ambavyo ni vichafu kusugulia kinembe (*pleasure knob*). Uelewa wa mwasilishaji wa mazingira na muktadha amba wengi wao ni wafugaji ulimsaidia kuteua istilahi hii ya *Foot and mouth*. Hii ni kwa sababu ng'ombe, mbuzi, kondoo na punda wanapokaa mahala pachafu huambukizwa ugonjwa huu katika kwato zao. Ugonjwa huu husababisha wanyama kushindwa kutembea na hata kwato zao kuozeana. Kutokana na uelewa huu mwasilishaji aliweza kuteua istilahi

hii ya tasfida *Foot and mouth* kuonyesha ugonjwa huu unaweza kumwadhiri mwanamke katika uke wake ikiwa usafi wa vidole vyatya mwanamume hauzingatiwi wakati wa kujamiiiana. Aligundua kuwa vidole vyatya miguu ya mwanamume lazima vifanyiwe ‘*pedicure*’ ili vinapotumiwa kusugulia kinembe (*pleasure knob*) visisababishe maradhi yoyote kwa mwanamke.

#### **4.4 Usawiri wa Jinsia katika tafsida**

Katika utafiti wetu tuligundua kuwa tasfida zilizotumiwa na mwasilishaji wa kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24 zinamdhalihsa mwanamke ilhali zinazomrejelea mwanamume, zinamkuza na kumwonyesha mtu wa kuheshimika na mwenye hadhi katika jamii. Katika istilahi za kumrejelea mwanamume mwasilishaji alitumia istilahi mbili muhimu ambazo ni *Mr Victor* na Safari fupi.

**Kiamb. 14:** *Mr Victor is what men carry between their legs, you know we are trying to be nice and we do not want to offend anybody. (Mr Victor ni kile wanaume hubeba katikati ya miguu yao, unajua tunajaribu kuwa wazuri na hatutaki kuudhi yeyote.)*

*Mr Victor* inamaanisha Bwana Mshindi, Kuwa sehemu ya siri ya mwanamume (dhakari) lazima iibuke mshindi, kwa kuipa jina la Bwana Mshindi ni dhihirisho la uwezo amba mwanamume amepewa katika jamii na hadhi yake ya juu. Kwa Kutumia istilahi *Mr Victor* ni dhihirisho la kuonyesha kuwa mwasilishaji anaolewa jamii zetu za Kiafrika ambazo huegemea kuume. Mwanamme huonekana mwenye nguvu na wakati wote husawiriwa kuwa mshindi. Hata kama ana udhaifu kidogo anaolezwa kichanya kwa sababu ya uume.

Ili kuwe na mshindi lazima kuwe na mshindwa na pia kuwe na vita. Mwasilishaji anaonyesha kuwa kujamiiiana ni kama vita ambavyo lazima mwanamume afaulu kwa kuibuka mshindi kupitia dhakari yake. Lazima mwanamume awe na uwezo wa kumpiga mwanamke kwa kutumia dhakari yake viliyvo kama ishara ya ushindi. Ule ugumu, udhabit, ukubwa na nguvu ya dhakari wakati wa mchechemo ni dhihirisho la uwezo wa mwanamume. Dhakari ni silaha ambayo mwanamume anafaa kutumia kuonyesha ushujaa wake dhidi ya mwanamke. Mwasilishaji alielezea kuwa lazima mwanamume achungwe na alishwe vyema ili aweze kuwa na nguvu wakati wa kujamiiiana. Hii inamaanisha kuwa ili dhakari iwe mshindi lazima ishughulikiwe na mwanamke kwa kumlisha mwanamume vizuri kwa chakula kifaacho ili apate nguvu. Tuligundua kuwa hili lilidhihirika kwa mwasilishi kutoa mafunzo kwa wanawake jinsi ya kuwalisha waume zao.

**Kiamb. 15:** *I have been getting lots of sms and calls; many people complaining of safari fupi (i.e premature ejaculation) or people taking longer.*  
(Nimekuwa nikipokea simu na jumbe nyingi watu wakilalamikia safari fupi yaani kumwaga manii mapema au watu kuchukua muda mrefu.)

Safari fupi inamaanisha kumwaga manii kabla ya wakati unaofaa (premature ejaculation). Kwa kawaida kumwaga manii mapema ni dhihirisho la udhaifu alionao mwanamume yejote yule, lakini kwa sababu ya mila na desturi ambazo haziruhusu mwanamume kutwezwa katika jamii, mwasilishaji alijaribu kutafuta istilahi inayopuuza yale makali ya udhaifu. Kule kupunguza makali kwa mwasilishaji kwa kutumia safari fupi ni dhihirisho tosha kuwa alifahamu nguvu na uwezo aliopewa mwanamume katika jamii hasa ya Kiafrika. Swala la mwanamme kumwaga manii kabla ya wakati ufaao ni aibu na ni dhihirisho la udhaifu kwa mwanamme na linaweza hata kusababisha talaka. Lakini jambo hili linachukuliwa kimzaha na mwasilishaji.

Jinsia imesawiriwa na mwasilishaji kwa kutumia istilahi nyingi ambazo zinadhalilisha mwanamke na kumwonyesha kama kiumbe cha hadhi ya chini. Katika sehemu hii tumejadili istilahi za tasfida zinazoegemea uke na kuonyesha jinsi zinavyomtweza mwanamke.

**Kiamb. 16:** *You should not care or worry about your dashboard, if it is small or big it does not matter.* (Usijali wala usishughulike kuhusu ‘*dashboard*’ kama ni ndogo au kubwa haijalishi).

*Dashboard* ni sehemu ya mbele ya gari ambayo huwa na vidhibiti mwendo, vipima kasi, masafa, joto, kiasi cha mafuta, duara la kuendesha gari na hata sehemu ya redio. *Dashboard* mwasilishaji anaitumia kama tasfida ya matiti. Kwa kutumia matiti kama *dashboard* mwasilishaji ameonyesha kwamba mwanamke ni kama gari ambalo lafaa kuendeshwa na dereva hapa akiwa ni mwanamume, kwa kupapasa matiti ya mwanamke, mwanamume alipewa uwezo wa kumdhibiti mwanamke apendavyo. Kwa kutumia matiti ya mwanamke kama *dashboard* ni ishara ya kumtweza mwanamke kwa kumlinganisha na gari.

**Kiamb. 10:** There are so many types of burners; an electric burner and a coal burner.  
This is a charcoal burner. chetezo kidogo cha makaa. (Kuna aina nyingi ya chetezo; kuna chetezo cha umeme na chetezo cha makaa. Hiki ni chetezo kidogo cha makaa, chetezo kidogo cha makaa.)

*Charcoal burner* ni aina ya chetezo kinachowashwa kwa kutumia aina fulani ya kemikali au makaa (*Vanilla*) na husaidia kunukiza harufu ya *Miss Victoria* ili kumvutia mwanamume. Chetezo linaanisha joto la uke (miss Victoria). Uke (miss victoria) inafaa kuhifadhi joto kwa muda mrefu kama vile chetezo huhifadhi joto. Kwa kutumia chetezo hiki ni dhihirisho la

kumtweza mwanamke, hii ni kwa sababu mwasilishaji hakutuonyesha kifaa chochote cha mwanamume kutumia ili kumvutia mwanamke. Itikadi za kitamaduni zimemtawala mwasilishaji kiasi cha kuona kuwa mwanamke ni chombo cha kumvutia mwanamume na ni jukumu la mwanamke kuhakikisha kuwa amemnasa mwanamume kwa kunukiza *Miss Victoria* yake. Kwa nini kusiwe na *Charcoal burner* ya kunukiza Mr. Victor?

**Kiamb. 2:** *I smoke myself, my room and actually my husband associates this smell with Mombasa raha trip, you know he comes, I do abit of udi nakwambia za kikikuyu zinasimama.* (Ninajifukisha, nafukisha chumba change na kwa hakika mume wangu huhusisha harufu hii na safari ya *Mombasa raha*, unajua anapokuja na nimefukisha udi hupandwa na jazba za kikuyu)

*Smoking the House* ni kunukiza chumba ili kumvutia mwanamume. Chumba hapa inamaanisha Miss Victoria (uke). Katika utafiti wetu tuligundua kuwa ni jukumu la mwanamke kufanya awezavyo kumvutia mwanamume hasa katika kufanya chumba kiwe na harufu ya kumvutia. Katika ile harakati ya kunukiza uke, chumba pia hujaa harufu ya kuvutia.

Huku ni kumtweza mwanamke kwa kumfanya kama mtumwa wa kumvutia mwanamume kwa hali na mali. Kwa nini mwanamume asitumiwe kunukiza chumba badala ya mwanamke? Kujamiiiana kwatakikana kuchangiwa na pande zote mbili (mume na mke) lakini inapoonekana kuwa mwasilishi alimlemea mwanamke sana kama kigezo muhimu cha kuchochea mahaba ni kumdhaililisha.

**Kiamb. 17:** *When it comes to the pleasure knob, it is all about pressure, how much pleasure depends on you.* (Tunapozungumzia ‘*pleasure knob*’ inategemea nguvu utakayoitumia, raha inategemea nguvu utakayoitumia.)

*Pleasure knob* ni kisimi. Ni kinundu ambacho kikiguswa huibua msisimko wa kuvutia kimahaba kwa mwanamke. Kwa kukiita kisimi *pleasure knob* ni kumtweza mwanamke. Hii ni sehemu muhimu sana katika mwili wa mwanamke haihitaji kuitwa kinundu cha raha.

Kila sehemu ya mwili wa mwanamke ni muhimu na haihitaji sehemu zingine za mwili kudunishwa.

**Kiamb. 18:** *Men love to go to Mombasa raha but they forget to prepare. I want to talk about a driver. A good driver takes good care of the car, checks that the tyres, oil, supporting documents are well taken care of. (Wanaume wanapenda kwenda Mombasa raha lakini huwa wanasahau kujitayarisha. Nataka kuzungumzia dereva. Dereva mzuri ni yule anayeshughulikia gari lake, anaangalia tairi, mafuta na kuangalia vilivyo *supporting documents*.)*

*Supporting documents* ni sehemu za mwili ambazo ni makalio na kiuno. Sehemu hizi mwasilishaji alitumia istilahi *supporting documents* kuonyesha zinasaidia katika kuendeleza kujamiihana. Kwa kutumia istilahi hii ya vifaa vya kusaidia ni kudunisha sehemu fulani za mwili wa mwanamke. Kuonyesha sehemu hizi lazima ziwe zimenenepa ili kutosheleza kujamiihana. Kwa nini sehemu hizi ziitwe visaidizi? Kwa nini zisipewe istilahi chanya yaani zinazoonyesha uzuri? Hizi ni sehemu muhimu sana kwa mwili wa mwanamke na zinapopewa majina ya kusaidia inaonyesha jinsi mwanamke anavyodhalilishwa na mwasilishaji. Kwa nini asiziite sehemu za mwili wa mwanamume visaidizi? Tuligundua kuwa ingawa hakudhamiria kumdunisha mwanamke, katika matumizi yake ya istilahi ‘*supporting documents*’ alifanya hivyo labda bila kukusudia.

**Kiamb. 19:** *Now that you have known how to touch your juicy spots, now let me teach you how to touch your man. (Sasa kwa sababu umejua kushika ‘juicy spots’ zako, sasa ningetaka nikufunze jinsi ya kushika mume wako.)*

Juicy Spots ni sehemu za mwili wa mwanamke ambazo zinapoguswa huibua msisimko wa kimahaba kwa mfano, *dashboard* (matiti), *pleasure knob* (kisimi), Athi river (mapaja) na nyinginez. Juicy ni kitu kiowevu, kitamu na ambacho kinaweza kuliwa au kunywewa. Kwa hivyo mwasilishaji aliporejelea sehemu hizo zinazosisimua hisia za kimahaba juicy spots, alizilinganisha na chakula ambacho kinaweza kulika. Mwasilishaji aliporejelea sehemu hizo hivyo alionyesha jinsi alivyodhalilisha mwanamke. Kwa nini aziite sehemu hizo za mwili juicy spots, kwani sehemu hizo zinaweza kulika?

Je, kwa nini hakuzirejelea sehemu zozote za mwanamume hivyo? Kwani mwanamume hana sehemu ambazo ni juicy spot? Sehemu zote za mwili ni muhimu na zina majukumu yazo. Na mwasilishi aliporejelea sehemu zingine kama *juicy spots* na hasa za mwanamke alionyesha jinsi anavyoweza kutumiwa tu kama chombo cha mwanamume kujifurahisha. Hii ndiyo sababu iliyomfanya kutambulisha sehemu hizo za mwili kama juicy spots. Hata kama ilikuwa ni njia yake mwafaka ya kuwasiliana, tuligundua kuwa kwa kuzipa zile sehemu jina la juicy spots ni mbinu ya kudhalilisha mwanamke.

Jinsia pia imesawiriwa kwa istilahi za tasfida kuhusu mitindo ya kujamiiiana. Mitindo miwili ambayo mwasilishaji alitumia inadhihirisha ubaguzi wa kijinsia. Mitindo hii imedhalilisha mwanamke.

**Kiamb. 9:** *Many women like Nyambura, the missionary style ingawa there are other styles like kuchuna mboga, oiyee, rabbit. (Wanawake wengi wanapenda nyambura, mtindo wa kimishonari ingawa kuna mitindo mingine kama vile kuchuna mboga, oiyee, rabbit.)*

Nyambura ni jina la kawaida katika jamii ya Wakikuyu na hutumiwa kumrejelea mwanamke. Jina hili laweza kutumiwa kumwakilisha mwanamke yeyote yule katika jamii yoyote ile. Katika utafiti wetu tuligundua kuwa *Nyambura style* ni mtindo wa kizamani (uliopitwa na wakati) wa kufanya mapenzi.

Mtindo ambao unachosha na hauwezi kuleta raha yoyote katika kujamiiiana. Kwa hivyo kwa kutumia istilahi *Nyambura style* kuwakilisha mtindo wa kizamani ni kumdunisha na kumdhgilisha mwanamke, kwa nini mwasilishaji hakutumia jina la mwanamume kama vile Kamau, Wafula kuwasilisha hoja hiyo? Kwa nini alitumia jina la mwanamke kuwasilisha hoja isiyo na umuhimu sana? Hili ni dhihirisho la jinsi mwasilishaji ingawa ni mwanamke anavyowaona wanawake kama viumbe visivyo na umuhimu sana na vile vimetwezwa katika jamii hasa za Kiafrika, kwa hivyo mwasilishaji ameathiriwa na itikadi za Kiafrika ambazo zinamtweza mwanamke na kumkuza mwanamume. Hivi kwamba mwanamume alihuishwa na mambo mazuri na mwanamke alihuishwa na mambo mabaya.

Kuchuna mboga ni mtindo wa kufanya mapenzi kama mbwa na ni mtindo ambao si mzuri sana. Tuligundua kazi ya kuchuna mboga hasa huwa ni ya wanawake katika jamii za Kiafrika. Watu wengi huchukulia kazi hiyo si nzuri na ambayo huchosha na ni vigumu sana kumpata mwanamume katika jamii za Kiafrika akifanya kazi hiyo. Kwa kutumia kuchuna

mboga kama mtindo mojawapo wa kujamiihana ni kumtweza na kumdunisha mwanamke. Ni kudhalilisha kazi ambayo wanawake huwa wanafanya ili kulisha familia zao, kwa nini mwasilishaji hakutumia istilahi za kudhalilisha kurejelea kazi zinazofanywa na wanaume kama vile uhunzi, uashi, uhandisi na kadhalika.

**Kiamb. 7:** *Today we decide to take a personal car to Mombasa raha we are taking a Mercedes Benz. For you to use a Mercedes Benz to go to Mombasa raha you do not just jump into the car and drive off and if you do hautafika mahali nakwambia utaishi njiani labda hata Athi river, you may be lucky if you fika Athi river maybe Mlolongo. (Leo tumeamua kuchukua gari la kibinagsi kwenda Mombasa raha, na tunachukua Mercedes Benz. Ili utumie Mercedes Benz kenda Mombasa raha hauwezi kuingia gari tu na kuondoka, ukifanya hivyo hautafika mahali, utaishia njiani labda athi river kama utabahatika labda utafika tu mlolongo.)*

Mercedez Benz ni gari muhimu la kifahari na lenye nguvu nyingi. Mtu mwenye gari hili huonekana mtu wa maana na wa kuheshimiwa. Mwasilishaji alitumia tasfida hiyo kurejelea mwili wa mwanamke. Alitaka kuonyesha thamani ya mwili wa mwanamke kama sehemu au kiungo muhimu katika kujamiihana. Kwa mwasilishaji kueleza mwili wa mwanamke kama Mercedez Benz ni kumdhilisha ingawa ni gari la kifahari, kumchukulia mwanamke kama gari linaloendeshwa na mwanamume vile apendavyo ni makosa.

Kwa kumlinganisha mwanamke na gari ni kumdhilisha au kumdunisha. Swali tulilojiuliza ni kwa nini hakumpa mwanamume jina kama vile dereva? Hii ni kwa sababu kukiwa na gari lazima kuwe na dereva. Gari huwa muhimu wakati mtu anataka kusafiri tu, akikamilisha safari yake gari huegezwa na mwenyewe kwenda kujishughulisha na mambo yake na akimaliza shughuli zake analirejelea na kurudi alikotoka. Tuligundua kuwa mwasilishaji kuupa mwili wa mwanamke jina `Mercedes Benz` ni kumtweza mwanamke kwa kuwa mwili ule utakuwa wa maana tu wakati wa kujamiihana na mwanamume anapokamilisha haja yake kuna uwezekano wa kumwona mwanamke kama mtu ambaye si wa maana sana. Kuna uwezekano mwasilishaji alidhamiria mema alipouita mwili wa mwanamke Mercedes Benz, lakini kwa kweli tuligundua kuwa uteuzi wake wa tasfida hiyo ulichangia kumsawiri mwanamke visivyo au kihasi.

Ili gari la aina ya *Mercedes Benz* kudumishwa vizuri lazima liwekwe mafuta ya kutosha na lishughulikiwe vizuri. Jambo hili la kuwafunza wanawake kuchunga miili yao lilifaa lakini angeweza pia kuwafunza wanaume jinsi ya kuwashughulikia wake wao angalau asionekane kana kwamba alikuwa akiegemea upande mmoja.

**Kiamb. 3:** *I am buying you a car Mombasa raha first class , no, kamata bonnet, bonnet can only be a car.(Ninakununulia gari Mombasa raha first class,la, shika bonneti, boneti inaweza tu kuwa gari)*

Boneti ni sehemu ya mbele ya gari iliyo na vifaa muhimu ambavyo husaidia gari kusonga. Bila boneti kuwa sawa gari haliwezi kusonga, kwa hivyo bonnet ni muhimu sana. Kukamata bonnet ni ile hali ambayo mwanamume huanza kumpapasa na kumshika mwanamke katika ‘juicy spots’ yaani sehemu za mwili kama vile matiti (*dashboard*), kisimi (*pleasure knob*), makalio na kiuno (*Supporting documents*) na sehemu nyinginezo ambazo huibua hisia za kimahaba kwa mwanamke. Mwasilishaji anapozungumzia kukamata bonnet kunadhihirisha jinsia. Mwanamume anakuzwa na mwasilishaji kwa kupewa uwezo wa kumsisimua mwanamke kwa kugusa sehemu mbalimbali za mwili wa mwanamke. Swali ambalo tulijiuliza ni Je, kwani mwanamume yeze hawezi kusimuliwa hisia za kimahaba na mwanamke kwa kumshikashika sehemu kama vile *Mr Victor*? Mwasilishaji alimduunisha mwanamke kwa kutompa nafasi sawa na mwanamume za kusimua hisia za kimpenzi.

Pia kule kuanza kwa mwanamume kumshikashika au kumpapasa mwanamke kuitwa au kupewa istilahi ya ‘Kamata Bonnet’ ni kumdhaliisha mwanamke. Kwa nini kitendo hiki cha kumpapasa mwanamke kilinganishwe na Kukamata Bonnet. Mwanamke hapa analinganishwa na gari vile linavyowashwa na kuendeshwa na dereva. Swali tulilojiuliza ni Je, kwani mwanamke ni gari? Mwanamume anapewa uwezo wa kuwa dereva na kuweza kumdhibiti mwanamke kama vile adhibitivo gari, kwa hivyo mwanamke ni kama gari.

**Kiamb. 20:** *What do people do to tamper with Miss Victoria PH? (Watuhufanya nini ili kuathiri kiwango cha joto cha Miss Victoria.)*

*PH* ni kiwango au kipimo cha asidi (ukali) au alkalini katika kitu fulani. Mwasilishaji alieleza *Miss Victoria PH* kama kiwango cha joto cha uke wa mwanamke. Mwasilishaji alitoa mafunzo kwa wanawake jinsi wanavyoweza kuimarisha kiwango cha joto katika uke wao kwa kuondoa baridi ambayo ingeweza kuwafukuza waume zao. Tuligundua kuwa

mwasilishaji alitilia maanani sana kuwafunza wanawake kuhusu kuhifadhi ile joto ya uke wao ili kuwafurahisha na kuwatosheliza waume wao. Kwa mwasilishaji kusitizia mwanamke kudumisha ‘*Miss Victoria PH*’ ni kumdhalihsa, kwani mwanamume yeze hawezi kuhifadhi kiwango cha joto cha *Mr Victor*? Mwanamume alipewa nafasi kubwa sana kuwa lazima atoshelezwe na mwanamke kwa hali na mali. Huku ni kumkuza mwanamume na kumdunisha mwanamke. Imani hii ya kuwa mwanamke lazima amtoshelezwe mwanamume kimpenzi inaendeleza unyanyasaji wa jinsia ya kike ilhali inampa mwanamume nafasi kubwa na kuonyesha uwezo alionao katika kutoa uamuzi katika familia. Uwezo huu wa mwanamume unapigiwa muhuri na itikadi za jamii mbalimbali. Tuligundua kuwa uelewa huu wa mwasilishaji wa itikadi hiyo, ulimsaidia kutoa mafunzo kwa wanawake jinsi ya kuimarisha kiwango cha joto ya uke wao.

**Kiamb. 21:** *My favourite incense is called Vanilla. It’s like sugar crystals, some powder or chunky cakes.* (Manukato ninayoyapenda zaidi huitwa *Vanilla*. Huwa ni kama sukari iliyoshikana, ungaunga au kiki.)

*Vanilla* ni kifaa chenye kemikali iitwayo ‘Vanillin’ ambayo hutoa harufu nzuri na kukifanya chakula kiwe kitamu. Wapishi wengi hutumia *Vanilla* kukipa chakula ladha. Mwasilishaji alitumia *Vanilla* na kuelezea kuwa ni kifaa cha kunukia. Tuligundua kuwa sababu za kunukiza *Miss Victoria* ni kumvutia mwanamume. Mwasilishaji alielezea kuwa mwanamke anafaa awashe chetezo kwa kutumia lavani, aweze kuchuchumaa na ule moshi upenyeze kwenye *Miss Victoria* na kufanya uke kutoa harufu nzuri yenyeye mvuto kwa mwanamume.

Ile hali ya mwasilishaji kuelimisha mwanamke katika matumizi ya lavani au *Vanilla* kumvutia mwanamume ni kumdunisha mwanamke. Kwa nini kusiwe na Lavani ya kunukiza Mr. Victor? Tunaelewa kuwa kuna marashi tofauti ambayo mengine hutumiwa na wanaume. Je, kwa nini mwasilishaji asingeshauri wanaume wanukize Mr. Victor zao ili kuwavutia wanawake kwa mwasilishaji kutoa ushauri wanawake wanukize *Miss Victoria* zao kwa ajili ya wanaume ni kuwafanya kama watumwa na kama chombo cha kutumiwa kuwafurahisha waume zao. Swala hilo la mwanamke kutumia *Vanilla* kunukiza *Miss Victoria* kwa ajili ya mwanamume ni la kumdhalihsa mwanamke na kumfanya awe mtumwa wa kuwa kivutio kwa mumewe kila wakati wa tendo la ndoa. Kwa nini mwanamume asitumie *Vanilla* ili awe kivutio kwa mwanamke? Pia lile swala la mwanamke kulazimika kutumia Vanila kunukiza Miss. Victoria ni kumpunguza na kumfanya kama kwamba yeze ni chakula cha mwanamume na ndiposa katika jamii nyingi za kiafrika

utasikia wanajamii wakirejelea kujamiana kama mlo. Tuligundua kuwa mwanamke ndiye huliwa na inabidi awe mtamu ndiposa mwasilishaji alitoa ushauri kwa mwanamke, kunukiza Miss. Victoria yake ili ‘alike’ vema na mwanamume. Hilo lilikuwa dhibitisho la jinsi jamii inavyomdhalihsa mwanamke na kumkweza mwanamume.

**Kiamb. 13:** Assuming that this is my husband and am going to borrow his toe, but by the time you put this toe in there , you better been have a pedicure otherwise you give *Miss Victoria foot and mouth* disease, you ndont need this to happen. (Nikichukulia kuwa huyu ni mume wangu na ninaazima kidole chake, lakini kabla hujatia hicho kidole ndani pale, ni afadhali uwe umeshafanya *pedicure*, la sivyo utampa *Miss Victoria* ugonjwa wa miguu na mdomo ilhali hutaki hili kutendeka.)

*Pedicure* ni kule kutengeneza na kutibu miguu kwa kukata kucha, kuzipaka rangi na kusugua ngozi iwe nyororo. Tuligundua kuwa kwa kawaida ngozi ya mwanamume huwa ngumu na pia wao hawashughulikii usafi wa kucha na vidole kama vile wanawake wafanyavyo. Kulingana na mila na desturi mwanamume hafai kuwa na ngozi nyororo na kutengeneza kucha kama mwanamke. Kwa mwasilishaji kupendekeza usafi huu ufanywe ni dhihirisho la uwezo alionao katika uelewa wake na mambo.

Alielewa fika kuwa wanaume wasipotilia maanani usafi wa kucha na usuguaji wa vidole viwe vyororo vinaweza kusababisha majeraha au magonjwa, vidole hivyo vikitumiwa kusugua *pleasure knob*. Uwezo wa mwasilishaji ulijitokeza anapoonekana akiwashawishi wanawake wawafanyie waume wao *pedicure* kwa usalama wao wenyewe. Uelewa wa mwasilishaji wa itikadi ulimsaidia sana kuweza kutoa mafunzo kuhusu ‘*Pedicure*’ kwa wanaume ili kuhakikisha usafi na kuzuia ueneaji ya magonjwa ambayo yanaweza kuepukika.Kule kumueleza mwanamke amfanyie mwanaume pedicure ni kumdunisha.Kwa nini mwasilishaji asimueleze mwanaume ajifanyie pedicure? kwa nini amuongezee mwanamke jukumu jingine la kumfanyia mwanaume pedicure? Hizi ni dhuluma na hazifai kuendelezwa katika jamii.

**Kiamb 22.** *I hope you are not tying a ponytail because if you do, you will not be comfortable.* (Natumai haujafunga aina ya nywele iitwayo ‘ponytail’ kwa sababu kama umeifunga hutakua mtulivu au sawa.)

*Ponytail* ni aina ya nywele ambazo wanawake husuka. *Ponytail* hapa inatumika kumaanisha pubic hair. Hizi ni nywele ambazo hukua sehemu zote za siri iwe ni mwanaume au mwanamke. Ingawa mwasilishaji alizungumzia kuhusu ‘*ponytail*’ akifunza mwanamke jinsi ya kunukiza ‘*Miss Victoria*’, anadhihirisha jinsia. Kwa nini iwe ni mwanamke awe amesuka ‘*ponytail*’, je mwanamume hawezi kuwa na hizo *ponytail*? Huku ni kumdunisha mwanamke na kuonyesha jinsi asivyozingatia usafi wa mwili wake. Asilimia kubwa ya wanawake hunyoa hizo nywele za sehemu ya siri hivyo hatukutaraji angeweza kuhusisha *ponytail* na wanawake pekee.

#### 4.5 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu umebainisha na kujibu maswali yote za utafiti tuliyoyaorodhesha katika sura ya kwanza. Tasnifu hii imebainisha wazi kuwa Kuna istilahi za tasfida za kujamiiiana zinazotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24 na zimetolewa maeleo mwafaka ili zieleweke kwa urahisi. Maeleo yaliyotolewa yalikuwa rahisi na ya kueleweka kwa urahisi. Kwa mfano, mwasilishi anaposema, ‘*Miss Victoria* is what women carry in between their legs,’ isingelihitajika kuwaza sana ukitafuta ni nini hiki mwanamke hubeba katikati ya miguu. Ni suala wazi na kueleweka haraka. Tasfida nyingi zilizotumiwa katika utafiti huu zilikuwa zkiegemea uke, hii ni kwa sababu katika matini tulizozitumia tasfida nyingi zilikuwa za kumrejelea mwanamke. Kulingana na madhumuni ya pili ya utafiti wetu, kuonyesha jinsi tasfida hizo zinasawiri jinsia, ilijitokeza wazi kuwa mwasilishaji alitumia tasfida nyingi kwa kuwarejelea wanawake ikilinganishwa na wanaume. Pia kutokana na mahojiano kati ya Mtafiti na mwasilishaji, tuligundua kwamba kipindi hiki kilidhamiria kutoa mafunzo mengi kwa wanawake na ndiposa mwasilishaji akawa anatumia tasfida nyingi kurejelea mwanamke. Tuligundua kuwa tasfida zilizotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24, zilikuwa za maneno ambayo ni mwiko na hayapaswi kutajwa hadharani na yaliyohusiana na kujamiiiana tu. Tulishughulikia yale ya kujamiiiana pekee kwa sababu lengo la kwanza la utafiti wetu ilikuwa ni kutambua na kueleza tasfida za kujamiiiana zinazotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24.

Tuligundua kuwa mwasilishaji alitumia tasfida katika uwasilishaji wake ili kuhifadhi heshima na kutofedhehesha watazamaji wake. Pia tulibaini kua tasfida zilizotumiwa ziliwiana vyema na itikadi na mazingira ya wakenya. Jambo ambalo lilirahisisha uelewaji kwa watazamaji.

Lengo letu la pili la utafiti huu lilikuwa kujadili swala la jinsia katika tasfida za kujamiihana zinazotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24. Katika uchanganuzi wa data tuliyokusanya tulibaini kuwa tasfida za kujamiihana zilizotumiwa zimesawiri jinsia hivi kuwa zinamkuza mwanamme kwa kumsawiri kichanya na kumtweza mwanamke kwa kumsawiri kihasi. Kwa mfano, sehemu ya siri ya mwanamme ilionyeshwa kama yenye uwezo na lazima iibuke mshindi na ndiposa ilipewa jina *Mr. Victor* yaani bwana mshindi. Tasfida zilizorejelea mwanamke zilikuwa zile za kudhihirisha majukumu yao ya kawaida kama vile kuchuna mboga na kuzisawiri kihasi kuonyesha kuhalalisha kwa hali ya kudunishwa kwa mwanamke. Katika uchanganuzi wa tasfida hizo ilidhihirika wazi kuwa mwanamke ni chombo cha kumfurahisha mwanamume. Kwa kufukisha nyumba kwa udi kumvutia mwanamume ni dhihirisho tosha. Kwa ujumla tasfida zilizotumiwa zilisawiri jinsia ya kike kihasi ilhali mwanamme alisawiriwa kichanya. Hali hii inaweza kuendeleza inyanyasaji wa jinsia ya kike kupitia lugha. Hata hivyo tasfida ni muhimu katika kukidhi mawasiliano miongoni mwa wanajamii na inabidi wanajamii wajifunze matumizi ya tasfida ili wajiepushe na Luga ya aibu.

## **SURA YA TANO**

### **MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

#### **5.1 Utangulizi**

Sura hii imejadili kwa muhtasari matokeo ya utafiti na mapendekezo ya tafiti za baadaye. Tasnifu hii imebainisha kuwa tasfida za kujamiihana zimetumika kwa wingi katika kipindi cha *Connect* cha Runinga ya K24. Tasfida hizi zimetumika kurejelea uume, uuoke, mitindo au jinsi ya kujamiihana, tendo la kujamiihana na istilahi nyinginezo. Istilahi hizi za tasfida zimetumika badala ya kutumia lugha ya mwiko. Hata hivyo istilahi hizi za tasfida kurejelea uume, uuoke na mitindo ya kujamiihana zimesawiri jinsia hivi kwamba zimemtukuza mwanaume au jinsia ya kiume huku zikimsawiri mwanamke kwa njia hasi au kumdhaliilisha mwanamke. Matokeo ya utafiti yanetokana na madhumuni ya utafiti yaliyoorodheshwa katika sura ya kwanza. Mahitimisho na mapendekezo yanatokana na matokeo ya utafiti.

#### **5.2 Muhtasari wa Tasnifu**

Tasnifu hii imeshughulikia istilahi za tasfida za kujamiihana zinazotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha Runinga ya K24. Azma ya utafiti huu ilikuwa kupambanua na kubainisha istilahi za tasfida za kujamiihana zilizotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha Runinga ya K24, kuzitaja na kuzitolea maelezo na kujadili jinsi tasfida hizo zilivyosawiri jinsia. Utafiti ulifanikishwa kwa matumizi ya nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi (UHU). Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi ina mihimili mitatu, uhakiki, itikadi na uwezo na inasisitiza matumizi ya lugha katika muktadha maalum.

Baada ya kuchanganua tasfida za kujamiihana zinazotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha K24, ilibainika wazi kuwa kuna tasfida za kujamiihana katika kipindi cha *Connect* cha K24 na matokeo yake ni kuwa zinarahisisha mawasiliano. Tasfida hizo ziliteuliwa kutoka mazingira nyeti na kuegemea itikadi zetu za waafrika. Kutokana na hayo uteuzi wa tasfida hizo ulirahisisha kueleweka. Utambuzi wa tasfida hizo ulikuwa wazi katika miktadha ya mazungumzo ya mwasilishaj wa kipindi hicho cha *Connect*. Maelezo ya tasfida hizo mengine yaliweza kutolewa na mwasilishaji moja kwa moja ingawa mengine yalijitokeza katika mazungumzo yake. Uchanganuzi huo wa tasfida za kujamiihana pia ulibaini kuwa swala la jinsia liko wazi hivi kwamba tasfida hizo zinamsawiri mwanamke kihasi na kumwonyesha kama kiumbe dhaifu na cha kudunishwa ilhali mwanamme amesawiriwa

kichanya na kupewa nafasi kubwa katika jamii. Tasfida ambazo ziliteuliwa kuhusiana na mwanamme zilikuwa zile za kumkuza kinyume na zile za wanawake ambazo zilimtweza. Mwanamme alisawiriwa kama mwenye nguvu na uwezo na chochote ambacho kingemsawiri vingine kisingekubalika kutumika.

Uwezo wa mwanamume ulijitokeza pia katika maelezo yake, anapoeleza wanawake jinsi ya kujichunga ili wawe kivutio kwa waume wao.

### **5.3 Hitimisho**

Kutokana na matokeo ya utafiti, ni dhahiri kuwa istilahi za tasfida za kujamiihana zimetumika kwa wingi katika kipindi cha *Connect* cha Runinga ya K24. Tasfida nyingi zilizotumiwa ni zile za kumrejelea mwanamke ilhali tatu tu zilitumika kumrejelea mwanamme. Istilahi hizi za tasfida za kujamiihana zimetumika kurejelea sehemu za siri za mwanamume na mwanamke, mitindo ya kujamiihana, tendo la kujamiihana lenyewe na istilahi nyingine. Istilahi hizi za tasfida hutumiwa kupunguza makali ya maneno hasa watu wanapojadiliana kuhusu swala la kujamiihana. Istilahi hizi za tasfida zimesawiri jinsia ya kike kwa njia hasi huku zinazorejelea jinsia ya kiume kwa njia chanya. Haya yametokana na mielekeo, imani, itikadi, matarajio na mitazamo ya jamii za Kiafrika.

### **5.4 Mapendelekezo**

Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha wazi kuwa kuna tasfida nyingi za kujamiihana zilizotumiwa katika kipindi cha *Connect* cha Runinga ya K24. Hata hivyo istilahi hizi za tasfida zimemsawiri mwanamke kwa njia isiyofaa au kwa dharau. Istilahi zilizotumika kurejelea mwanamume ni zile zakumkuza na kumwonyesha kama mwenye uwezo akilinganishwa na mwanamke ambaye ametwezwa na kuonyeshwa kama mdhaifu na chombo cha kumfurahisha mwanamume. Tunapendekeza tafiti zaidi zifanywe kuhusiana nalugha ya tasfida na jinsia katika jamii na katika vipindi mbalimbali vyta runinga na redio ili kuleta usawa wa kijinsia katika bara la Afrika. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa mwanamke ana uwezo wa kuelimisha, kutumia lugha vizuri na ni amiri mkuu wa kuleta mabadiliko katika jamii. Tunapendekeza tafiti zaidi zifanywe kuhusu uwezo na matumizi ya lugha kwa wanawake. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa maneno ya tasfida hutumiwa kurahisisha mawasiliano na kuzuia kufedhehesha katika mawasiliano. Tunapendekeza tafiti zaidi zifanywe kuhusiana na lugha ya tasfida katika vyombo vyta habari ili kurahisisha mawasiliano. Kwa kuhitimisha, ni matumaini yetu kuwa utafiti huu wetu utakuwa kichocheo kwa wasomi wanaotafiti katika nyanja za lugha, jamii na utamaduni.

## **MAREJELEO**

Abudi, M. (2011). *Language, Gender and Power Relations*. Egerton University: Unpublished M.A Thesis

Adei, S. (1991). *The Secret of a Happy Marriage: Communication*, African Christian Press.

Adler, R. & Rodman, G (2003). *Understanding Human Communication*. New York: Oxford University Press.

Akmajian, A. Demers, R. Farmer, A. & Harnish, R. (2001). Linguistic: *An introduction of language and communication*, Cambridge: MIT press.

Allan.K. & Burridge, K. (2006). *Forbidden Words: Taboos and the Censoring of language* Cambridge, Cambridge University press.

Ambuyo, B. Asiko, (2011). *Face Threatening Acts and standing orders: “Politics” in the Question Time Discussion of the Kenyan Parliament*. International Journal of Humanities and Social Science.Vol 1 NO. 9- Special issue.

Arowgulu, A. (2002). *Sexuality: Contraceptive choice and AIDS Awareness among Nigerian undergraduate*. Africa Journal of Reproduction Health vol.6 No .2.

Aswani, B., Kimani, N., Alice M. (2006). *Isimujamii*. Nairobi: *Jomo Kenyatta foundation*:

Austian, J. L. (1962). *How to do things with words* Cambridge. Mass: Harvard University Press.

Baran, S. J., Mcntyre, J.S & Meyer, T. P. (1984). *symbols and society: An introduction of mass Communication*. California: Addison – Wesley Publisher company inc.

Berges, E., Neidebach, S., Rubin B. (1983). *Children and Sex: the Parent Speak*. New York: Facts on File.

Berlin, B. & Kay, P. (1969). *Basic Colour Terms: University and Evolution, Anthropology, Linguistic, Psyschology*. University of carlifornia.

Brown, P. & Levinson, S. (1987). *Politeness: Some Universals in Language Usage*. United Kingdom: Cambridge University press.

- Brown, G. & Yule, G. (1993). *Discourse Analysis*. Newyork: Cambridge University Press.
- Bucholtz, M. & Hall, K. (2004). *Theorizing identity in language and sexuality research*. *Language in Society* 33:469 - 515.
- Bucholtz, M. (2004). *Theorizing Identity in language and sexuality Research*. Cambridge: Cambridge University press.
- Butler, J. (1990). *Gender Trouble: Feminism and the subversion of identity*. London Rout ledge: Cambridge University Press.
- Cameron, D. & Kulick, D. (2003). *Language and Sexuality*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Carli, L. (1999). *Gender, interpersonal power and social influence*. *Journal of social issues* <http://www.BNET.htm> 15 April 2010. Chicago; university of Chicago press
- Connell, R. (2011). *Masculinity research and global society*. Pp. 51-72 in Esther Ngan-ling Chow.
- Choti, A. (1998). *The Linguistic Potrayal of the Gusii woman*. Egerton University: Unpublished MA Thesis.
- Comwall, A. & Jolly, S. (2006). (Eds). *Sexuality matters Journal of institution of development studies*. London: Warwick vol.37.No.5.
- Cory, D. (1951). *The homosexual in America- a subject approach*. New York: Greenberg.
- Crystal, D. (1992). *The Cambridge Encyclopedia of language Cambridge*. C.V.P. Cultural Prospective Palgrave Macmillan.
- David, O. (2006). *Usawiri wa Ubabe wa Mwanamume katika methali za Ekigusii*. Egerton University: Unpublished MA Thesis.
- Debatin, B. (2000). *Literature on the Theory of metaphor*. <http://www.unileipzig.de-debating/English>
- Debatin, B. (2000). *Literature on the Theory of metaphors*, <http://www.uni Leipzig-debating/English research/metaphor.htm> 28 July 2008.

Denasi, M. (2002). *Understanding media semiotics* Great Britain. norldresearch/metaphor  
htm 28<sup>th</sup> July 2008

Durkheim, E. (1995) *The rules of sociological method*. New York: Free press

Edinburgh Gate En Wikipedia org/wiki/critical – discourse – analysis *Experiences with Cancer. Health communication. Vol.14.NO.2*

Fairclough, N. (1989). *Language and power*. London: Longman.

Fairclough, N. (1991). *Language in the News: Discourse and Ideology in the British Press*. London: Routledge.

Fairclough, N. (ed.) (1992). *Critical Language Analysis*. London: Longman.

Fairclough, N. & Wodak, R. (1997). *Critical Discourse Analysis*. In Van Dijk T. (ed.) *Introduction to Discourse Studies*. Loss Angeles: Sage. PP.258-284

Fairclough, N. (1995). *Critical Discourse Analysis*. Boston: Addison Wesley.

Faucoult, M. (1979). *The history of sexuality Vol.1*. London, Allen lane, Paris (orig. 1976).

Foucault, M. (1978). *The history of sexuality*. New York: Pantheon.

Fowler, R. (1991). *Language in the News .Discourse and Ideology in British Press*. London: Routledge.

Greer, G. (2000). *The whole Women*. Anchor: London.

Grice, H. P. (1957). *Meaning* Philosophical review ,66,377- 388 (1997) *logic and conversation* in P. Cole and J.H Morgan (Ed) syntax and semantics vol,3.speech acts (pp.41 – 58) New York Academic press.

Gumperz, J. (1982). *Discourse strategies*. Cambridge University press.

Hall, K. & Bucholtz, M. (ed) (1995). *Gender articulated language and the society constricted self*. London: Routledge.

Haralambos, M. Holborn, M. & Heald, R. (2008). *Sociology:Themes and perspectives* Harper- Collins Publisher Limited, London.

- Harris, Z. (1951). *Methods in structural linguistics*. Chicago: university of Chicago press  
University of Pennsylvania press.
- Hoey, M. (1991). *Patterns of Levis in text*. Oxford University press: Walton Street, New York.
- Huang, H. & Tian, G (1990). *A sociolinguistic view of linguistic Taboo in Chinese* in *International Journal of the sociology of language* 81.
- Hymes, D. (1974). *Foundations in sociolinguistics: An ethnographic Approach*. Philadelphia: University of Pennsylvania Press.
- Jay, T. King, K. & Duncan, D . (2006). *Memories of Punishment for Cursing. Sex Roles*, 32,123-133.
- Joseph, G.I & Lewis, J (1981). *Common differences: conflicts in black and white feminist perspective* Boston: South end press.
- Kress, G. (1985). *Linguistic process in socio-cultural practice*. Victoria: Deaken University Press.
- Kumar, K.J (2005). *Mass communication in India*. Jaico publisher house: Mahatma Gandhi Road.
- Kyrtzis, S. (2007). *The Semantics of Desire: Exploring Desire, Love and sexuality Through metaphors in sauntson* H & Kyrtzis, S. (2007). (Eds) languages, sexuality and Desire; cross – cultural perspective. Palgrave: Macmillan.
- Lakoff, C. (1974). *What you can Do with words. Politeness, pragmatics and performatives* Berkeley California.University of California.
- Leap, W. (ed.) (1995). *Beyond the lavender lexicon .Authentiality, magi nation & Appropriation in lesbian and gay language*.Buffalo .NY; Gordon and Breach.
- Leap, W. (1996). *Words out Gay men's English manmeapolis*:University of Minnesota press.
- Leap, W. and Boetlstorff, I. (Ed) (2004). *Speaking in Queer Tongwes: Globalization and gay language in urban* and Chicago University of Illinois press.

Leech, N.G. & Short. M. (1981). *Style in Fiction*: A linguistic introduction to English fictional prose. London: longman

Legman, G. (1941).*The language of Homosexuality*; an American glossary in Henry, G (ed) sex variety a study of Homosexual patterns, vol.2.London: Paul B. Hoeber inc.pp.1149-79.

Livia, A. & Hall,K. (E) (1997). Queerly phrased: language gender and sexuality Oxford :Oxford University.

Locher, M. (2004). *Power and Politeness in Action*. Moulton press: Berlin.London Tailstock.

Macionis, J.J & Plammer, K. (1997). *Sociology A global introduction person Education limited,*

Malinoswki, B. (1930). *The problem of meaning in primitive languages* In C. Ogden and I. A. Richard, The meaning of meaning of (2<sup>nd</sup> ed) London Routledge and kegan and Paul.

Manka D. (2011). *Interpretations of HIV&AIDS Television Advertisements Amongst Selected Secondary School Students in Njoro district Nakuru County*. MA Thesis Egerton University (Haijachapishwa)

Meyerhoff, M. (2006). *Introducing Socialinguistics*. London and New York: Routledge.

Moore, S & Rosenthal, D. (1993). *Sexuality in Adolescence*. London: Routledge publishers.

Mwanzandi, S. (2001). *Usemezano katika Taarabu*. PhD Thesis. Egerton University (Haijachapishwa).

Ndambuki J.M. (2010). *Discursive Representation of women's needs and interests*. Unpublished PhD Thesis. University Witwaterrand.

Ngara, E. (1982). *Stylistic critism and the African Novel*. London: Heinemann

Njenga, R.N .(2011). *The Discourse of Metaphors of Sexuality among Kenyan University students*. A case study of students from Egerton University: M. A. Thesis Egerton University (Haijachapishwa).

Noor, S. (1983). *Function of dialogue in Swahili society*. PhD Thesis university of New Jersey

Ontieri, J. O. (2005). *Uchanganuzi wa Matumizi ya Lugha Katika Magazeti ya Kiswahili Nchini Kenya*. Mfano wa Gazeti la Taifa leo, Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Egerton. (Haijachapishwa).

Onyango, J. O. (2011). *Discursive Masculinities and The War Against AIDS*: The Kenyan Experience, Division of Research and Extension, Egerton University.

Qing, L. (2005). On *Cooperative Principles and Politeness Principle in Diplomatic Language Strategy..*

Riro, M.S. (2006). *Usawiri wa Mwanamume Katika Nyiso za Jado Mionganii mwa Abakuria*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Egerton. (Haijapishwa).

Rodges, B. (1997). *The Queen's vernaculars a Gay lexicon*. Blond and Briggs.

Sanderson, P. (1999). *Using newspaper in the classroom*. The United Kingdom: Cambridge University Press.

Sauntson, H. & Kyrtzis, S. (ed) (2007). *Language sexuality titled the displacement of concept.*

Schiffrin, D. (1987). *Discourse markers*, press syndicate of the University of Cambridge.

Schiffrin, D (1994). *Approach to Discourse*. Oxford, Blackwell Publisher Ltd.

Searle, J.R. (1969). *Speech Acts*. Cambridge: Cambridge university press.

Simmel, G. (1961). *The sociology of sociability* In T. parson et.al. (eds.) Theories of society. New Delhi.

Stubbs, M. (1983). *Discourse Analysis*: the sociolinguistics analysis of natural language, *Studies*. London: Warwaick vol. 37. No. 5.

Taiwo, R. (2005). *Language ideology and power relation* in Nigeria Newspaper headlines, Lagos.

- Thomas, J. (1995). *Understanding social science*. UK: Black well.
- UNAIDS, (2000). Joint *United Nation Programme on HIV/AIDS*. Geneva: Switzerland.
- Undie, C. Crichton, J. & Zulu, E (2006). *Talking about sex using youth languages in sexual Education*. African Journal of reproductive Health Vol.11.NO.3
- Van Dijk, T. (1997). *Discourse as social Interaction*: Sage publication.
- Wodak, R. (1996). *Critical Linguistics & Critical Analysis*: Handbook of Pragmatics, Amsterdam, Benjamins.
- Wodak, R. (1999). *Introduction in R. Wodak (ed), Language power and Ideology*. Amsterdan Benjamins.
- Wodak, R. & Van Dijk, T.A. (eds.) (2000). *Racism at the top*. Parliamentary Discourse on Ethnics issues in six European states. Klagenfurt, Drava.
- Wodak, R. (2001). What CDA is about - *A summary of its History, important concepts and developments in R. Wodak and M Meyer (eds.) Methods of critical discourse Analysis: introducing Qualitative methods* London Thousand Oaks and New Delhi sage publications1-13.
- Wood, D. (1983). *Mass media and the individual*. Boulevard: West publishing co.
- World Health Organization (WHO) (2005). *The World Health Report*. Switzerland: Geneva.
- Zhenqiang, F. (2006). *The Mechanism of Euphemisms*. <http://www.linguistic.cn/doc>

## **VIAMBATISHO**

### **KIAMBATISHO A. MAHOJIANO**

Mahojiano ya Mtafiti kwa mwasilishaji wa kipindi cha *connect*

Jina langu ni anne njambi chege mwanafunsi wa uzamili katika chuo kikuu cha Egerton.

Ninatafiti kuhusu matumizi ya tasfida za kujamiihana na usawiri wa jinsia katika kipindi cha *Connect* cha runinga ya K24, Kenya

Madhumuni makuu ya utafiti huu nia kutaja , kueleza na kuonyesha usawiri wa jinsia katika tasfida za kujamiihana zinazotumiwa katika kipindi cha *Connect*. Habari utakazozitoa zinatumika tu katika utafiti huu.

#### **Maswali ya mahojiano**

1. Kwa nini kipindi hiki kiitwe *Connect*?
2. Kinahu nini hasa?
3. Madhumuni ya kipindi hiki *Connect* ni nini?
4. Kwa nini utumie tasfida?
5. Kwa nini kipindi hiki kiwasilishwe saa nne usiku?
6. Kipindi hiki kina athari gani kwa jamii?
7. Ni nini kilichokuchea kuanzisha kipindi hiki?

## KIAMBATISHO B

### TASFIDA ZA KUJAMIIANA ZILIZOTUMIKA

1. *Mombasa raha* being a place of happiness all want to go to *Mombasa raha*, isn't it? But the approach and *Mode of Transport* is different (Mombasa raha kuwa ni mahali pa furaha, watu wote wangependa kuenda *Mombasa raha* au siyo, lakini mtazamo na jinsi ya kusafiri ni tofauti.)
2. I smoke myself, my room and actually my husband associates this smell with *Mombasa raha trip*, you know he comes, I do abit of udi nakwambia za kikuyu zinasimama. (Ninajifukisha, nafukisha chumba change na kwa hakika mume wangu huhusisha harufu hii na safari ya *Mombasa raha*, unajua anapokuja na nimefukisha udi hupandwa na jazba za kikuyu)
3. I am buying you a car *Mombasa raha first class* , no, kamata bonnet, bonnet can only be a car.(Ninakununulia gari *Mombasa raha* first class,la, shika bonneti, boneti inaweza tu kuwa gari)
4. Men would prefer, you understand, to fly to *Mombasa raha* and when they fly they miss out so many things on the way. (Wanaume wangependa unaelewa kupaa kwenda *Mombasa raha* na wanapopaa wanakosa vitu vingi njiani)
5. Women on the other hand, would like to take a train, I mean how many hours, 12 hours and do you know how many stops on the way, I think over 10.(wanawake kwa upande ule mwingine wangependa kwenda *Mombasa raha* lakini wangependa kutumia gari la moshi, namaanisha masaa mangapi, kumi na mawili na unajua wanasimama mara ngapi njiani, nafikiria zaidi ya kumi)
6. You can compromise and take a personal car, there is so much you can do, you can determine the speed on the way, you can have stops on the way. Do you want to stop around ukambani area where you can buy

bananas, oranges, pawpaws, hohos or want to go straight down.(mnaweza kukubaliana na kuchukua gari la kibinafsi, kuna mengi mnaweza kufanya, unaweza kuamua kasi au mahala pa kusimama kule ukambani ambapo utaweza kununua ndizi, machungwa, paipai, pilipili hoho au unataka kwenda moja kwa moja chini)

7. Today we decide to take a personal car to Mombasa raha we are taking a Mercedes Benz. For you to use a Mercedes Benz to go to Mombasa raha you do not just jump into the car and drive off and if you do hautafika mahali nakwambia utaishi njiani labda hata athi river, you may be lucky if you fika athiriver maybe mlolongo. (Leo tumeamua kuchukua gari la kibinafsi kwenda Mombasa raha, na tunachukua Mercedes Benz. Ili utumie Mercedes Benz kwenda Mombasa raha hauwezi kuingia gari tu na kuondoka, ukifanya hivyo hautafika mahali, utaishia njiani labda Athi river kama utabahatika labda utafika tu Mlolongo.)
8. When you are checking the dashboard, just make sure everything is okay.(Wakati unaangalia ‘dashboard’ hakikisha kila kitu kiko sawa.)
9. Many women like Nyambura, the missionary style ingawa there are other styles like kuchuna mboga, oyee, rabbit . (Wanawake wengi wanapenda nyambura, mtindo wa kimishonari ingawa kuna mitindo minginekama vile kuchuna mboga, oyee, rabbit.)
10. There are so many types of burners; an electric burner and a coal burner. This is a charcoal burner.jiko ndogo ya makaa. (Kuna aina nyingi ya jiko; kuna jiko la umeme na jiko la makaa. Hili ni jiko la makaa, jiko ndogo ya makaa.)
11. Turn to reverse cow girl and of course he will love this because really the supporting documents look good. (Angalia nyuma na atapenda kwa kuwa the supporting documents zinakaa nzuri.)

12. *You oftenly hear a couple say oh he doesn't give me foreplay or she doesn't like foreplay.* (Mara nyingi utasikia wanandoa wakisema oh mume wangu hanipi ‘ a foreplay’ au mke wangu hapendi ‘foreplay’.)
13. Assuming that this is my husband and am going to borrow his toe, but by the time you put this toe in there , you better been have a *pedicure* otherwise you give *Miss Victoria foot and mouth disease*, you ndont need this to happen. (Nikichukulia kuwa huyu ni mume wangu na ninaazima kidole chake, lakini kabla hujatia hicho kidole ndani pale, ni afadhali uwe umeshafanya *pedicure*, la sivyo utampa *Miss Victoria* ugonjwa wa miguu na mdomo ilhali hutaki hili kutendeka.)
14. *Mr Victor* is what men carry between their legs, you know we are trying to be nice and we do not want to offend anybody. (*Mr Victor* ni kile wanaume hubeba katikati ya miguu yao, unajua tunajaribu kuwa wazuri na hatutaki kudhulumu yejote.)
15. I have been getting lots of sms and calls; many people complaining of safari fupi (i.e premature ejaculation) or people taking longer. (Nimekuwa nikipokea simu na jumbe nyingi watu wakilalamikia safari fupi yaani kumwaga manii mapema au watu kuchukua muda mrefu.)
16. You should not care or worry about your *dashboard*, if it is small or big it does not matter. (Usijali wala usishughulike kuhusu ‘*dashboard*’.)
17. *When it comes to the pleasure knob, it is all about pressure, how much pleasure depends on you.* (Tunapozungumzia ‘*pleasure knob*’ anategemea na nguvu utakayoitumia, raha inategemea na nguvu utakayoitumia.)
18. *Men love to go to Mombasa raha but they forget to prepare. I want to talk about a driver. A good driver takes good care of the car, checks that the tyres, oil, supporting documents are well taken care of.* (Wanaume

wanapenda kwenda *Mombasa raha* lakini huwa wanasahu kujitayarisha. Nataka kuzungumzia dereva. Dereva mzuri ni Yule anayeshughulikia gari lake, anaangalia tairi, mafuta na kuangalia vilivyo *supporting documents.*)

19. *Now that you have known how to touch your juicy spots, now let me teach you how to touch your man.* (Sasa kwa sababu umejua kushika ‘juicy spots’ zako, sasa ningetaka nikufunze jinsi ya kushika mume wako.)
20. *What do people do to tamper with Miss Victoria PH?* (Watu hufanya nini ili kuathiri kiwango cha joto cha *Miss Victoria* .)
21. *My favourite incense is called Vanilla. It’s like sugar crystals, some powder or chunky cakes.* (Manukato ninayoyapenda zaidi huitwa *Vanilla*. Huwa ni kama sukari iliyoshikana, ungaunga au kiki.)
22. I hope you are not tying a ponytail because if you do, you will not be comfortable. (Natumai haujafunga aina ya nywele iitwayo ‘ponytail’ kwa sababu kama umeifunga hutakua mtulivu au sawa.)
23. *Mombasa raha* is what men and women do in between the sheets. (*Mombasa raha* ni kile wanaume na wanawake hufanya ndani ya mashuka kwenye kitanda.)
24. *Miss Victoria* is what a woman carries in between her legs, you know there are things that never leave and never run out. (*Miss Victoria* ni kile mwanamke hubeba katikati ya miguu yake na unajua hivi ni vitu ambavyo haviondoki wala kuisha.)
25. You oftenly hear a couple say oh he doesn’t give me foreplay or she doesn’t like foreplay. (Mara nyingi utasikia wanandoa wakisema oh mume wangu hanipi ‘ a foreplay’ au mke wangu hapendi ‘foreplay’.)

26. Miss Victoria's smell keep changing, it sometimes smells good or bad, kama umekula maharagwe ama githeri, Miss Victoria atanuka githeri na maharagwe. Na wenzangu wa mijikenda you eat shark Miss Victoria smells shark. You do want to take a trip to Mombasa raha and your Miss Victoria is smelling shark. (harufu ya Miss Victoria habadilikabadilika, wakati mwingine inaweza kunukia na wakati mwingine kunuka vibaya, kama umekula maharagwe au githeri atanuka maharagwe au githeri. Na wenzangu wa mijikenda ukila 'shark' miss victoria atanuka 'shark'. Unataka kwenda safari ya Mombasa raha na Miss Victoria wako ananuka shark.)
27. There is something very interesting here about smoking Miss Victoria and the room. Coastarian take good care of Miss Victoria. (Kuna jambo la kufurahisha hapa kuhusu kufukisha Miss Victoria na chumba. Wanawake wa pwani wanajua kuchunga au kushughulikia 'Miss Victoria').
28. This is actually called the plough, when the guy is on top. The most common position is the plough; you can move your legs around. (Hii kwa hakika ndiyo inaitwa 'plough' ambapo mwanamume yuko juu. Mtindo ambao ni wa kawaida sana ni plough na unaweza kuzungusha miguu.)
29. The next position we are going to demonstrate is the T-position (Turn). You begin very slowly and then you build up. (Mtindo mwingine tutakaouonyesha ni 'T-position' unaanza polepole na kuendelea kuijenga.)
30. For the guys who watch true love and have said I have 360 position and a set off four. You have not gone to Mombasa raha until you try 360 position. (Kwa wale ambao hutazama 'true love' na wanasema niko na 360 positionna set of four. Hujaenda Mombasa raha mpaka ujaribu 360 position.)
31. I want to demonstrate something called a clitiche. What's a clitiche? Of course it comes from the word pleasure knob. (nataka kuonyesha kitu

kiitwacho ‘clitiche’. ‘clitiche’ ni nini? Kwa hakika linatokana na neon ‘*pleasure knob*’-kisimi.)

32. The katavali is where you massage or hit Mr. victor with a *pleasure knob*.  
(katavali ni wakati unapigapiga au guyisha ‘Mr. Victor’ kwa kisimu ‘*pleasure knob*’.)
33. When we talk of going to *Mombasa raha* we are talking of joining Mr. Victor and *Miss Victoria*. (Tunapoongea kuhusu kuenda *Mombasa raha*, tunaongea kuhusu kuunganisha *Mr Victor* and *Miss Victoria*.)